




**Kikongwe** matatani tuhuma za kuua mjukuu kwa jembe

UKURASA 16




UKURASA 11


# Nipashe

Jumatatu Septemba 4, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581423

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com 0745 700710 LIKE & FOLLOW US




Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi -Zanzibar Suleiman Masoud Makame

Waziri wa Mifugo- Abdallah Ulega

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe

MKUTANO MIFUMO YA CHAKULA

## Fursa tele hizi hapa

• **Dola** zilizoadimika zaletwa nchini, masoko ya bidhaa, neema yaja... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

**ATUPWA JELA MIAKA 30 KWA KUSAFIRISHA BANGI**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Morogoro imemhukumu Awadhi Mohamed, kwenda jela miaka 30 kwa kosa la...

UKURASA WA 4

**'VIRAKA' KATIBA 1977 VIZIBWE KABLA YA UCHAGUZI 2024/25'**

KITUO cha Demokrasia Tanzania (TCD), kimeishauri serikali kufanya mabadiliko madogo katika Katiba...

UKURASA WA 7

**CHADEMA YAPOKEA WAPYA 100 KUTOKA ACT, CCM, CUF**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo(CHADEMA) Kanda ya Kusini kimepokea wanachama wapya zaidi...

## Wasiojulikana wavunja kanisa, waiba sakramenti

UKURASA 3



Mhashamu Thomas Kiangia akiwekwa wakfu kuwa Askofu mpya wa Jimbo Katoliki la Tanga katika sherehe za kusimikwa zilizofanyika Chumbageni, jijini Tanga jana. **Habari Uk. 4. PICHA: OWM**

## Lissu aibuka na tuhuma nzito

• **Waziri** acharuka, amtaja Mbowe... *Ukurasa wa 2*

**MICHEZO** **MASTAA SIMBA WAIONYA AL AHLY AFL** UK.24 **KATUNI** UK.6



Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, akizungumza na waharir wa vyombo vya habari kuhusu Mkutano Mkuu wa Mifumo ya Chakula Afrika (AGRF-Afrika Food Systems Summit 2023) Ikulu jijini Dar es Salaam jana. Mkutano huo unatarajiwa kufanyika jijini Dar es Salaam kuanzia kesho. **PICHA: IKULU**

# Fursa hizi hapa Mkutano Mifumo ya Chakula Afrika

**Na Jenifer Gilla**

MAWAZIRI wa Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Uchumi wa Bluu, wameeleza fursa lukuki zitakazopatikana kwa Tanzania kupitia Mkutano wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika (AGRF) utakaoanza kesho hadi hadi Ijumaa ya juma hili.

Ni mara ya kwanza mkutano huo kufanyika nchini, ukiwavutia watu zaidi ya 3,300 wakiwamo marais saba, mawaziri, wakuu wa taasisi zaidi ya 500, watafiti, wafanyabiashara na sekta zote.

Katika mazungumzo na wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari nchini kupitia mkutano ulioandaliwa na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais Ikulu, Zuhura Yunus, jijini Dar es Salaam jana, mawaziri hao walisema watatumia mkutano huo kutafuta fursa na mbinu za kukuza sekta za mifugo, uvuvi, kilimo na utalii nchini.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alisema mkutano huo umebeba dhamira ya Rais Samia Suluhu Hassan kuzipa kipaumbele sekta zinazogusa watu wengi ikiwamo mifugo na uvuvi kwenye mitaji, masoko na teknolojia.

"Kutakuwa na wataalamu wengi kutoka nchi mbalimbali. Washiriki watapata nafasi ya kuingia katika mikutano midogo ambayo itasaidia kukuza kilimo, uvuvi na mifugo, biashara ambayo ina tija kwa watu wetu, tutawaleta vijana wa sekta hizo," alisema.

Waziri huyo alisema ni matarajio yake kuwa kupitia mkutano huo, vijana na wanawake watapata fursa ya kujifunza kutoka mataifa mengine kuhusu teknolojia ya kunenepesha mifugo ili ilete tija kwao na kukuza uchumi wa taifa.

Waziri wa Kilimo, Mifugo, Umwagiliaji na Maliasili Zanzibar, Shamata Shaame Khamis, alisema mkutano huo utatoa fursa mbalimbali kujifunza teknolojia ya kukuza na kuboresha mifugo ikiwamo kunenepesha ng'ombe ili kukidhi mahitaji ya nyama na maziwa.

Alisema mkutano huo pia utakuwa ni chanzo cha kutafuta masoko na teknolojia ya kuboresha na kuongeza thamani katika bidhaa zinazozalishwa Zanzibar, ikiwamo vanila na kutangaza utalii wa eneo hilo kama vile kuwa na popo wa kipekee. Hawapatikani maeneo mengine.

Alisema sekta ya kilimo inachangia Pato la Taifa kwa asilimia 22, huku asilimia 40 ya wakazi wa Zanzibar wanajishughulisha na kilimo na kunufaisha takribani asilimia 70 ya wakazi wake.

Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Samweli Shelukindo, alisema mkutano huo umetokana na juhudi kubwa za Rais Samia kuhakikisha nchi inajikita zaidi katika utalii wa mikutano na kukuza diplomasia ya uchumi.

Alisema ni mategemeo ya wizara hiyo kuwa mshiriki mmoja katika mkutano huo atatumia si chini ya Dola ya kimarekani 500 (Sh. milioni 1.248) na watakaotembelea jiji, waingize zaidi ya Dola 800 (Sh. milioni 1.998), hivyo kuwanufaisha wenye hoteli na kuiingizia nchi fedha za kigeni.

Waziri wa Uchumi wa Buluu Zanzibar, Suleiman Masood Makame, alisema vipaumbele vyao ni uvuvi na ufugaji wa mazao ya baharini, utalii wa bahari, mafuta na gesi, miundombinu ya usafiri wa bahari na usimamizi wa bahari.

Alisema miradi yote inayotekelezwa inalenga kuwawezesha vijana katika kuelimishwa, kupata mitaji, kupata na kuyafikia masoko kwa urahisi.

"Zanzibar ni ya pili kwa uzalishaji wa mwani na tunazalisha tani 15,000 na malengo ni tani 30,000. Bei ni Sh. 1,200 na kiwanda kikianza itafika Sh. 3,000," alisema.

Makame alisema zaidi ya vijana 2,000 wamewezeshwa katika kilimo cha matango bahari ambacho ni chakula kikuu duniani. Ni muhimu kwa ujenzi wa afya na kinga dhidi ya maradhi ya saratani. Kilo moja kwa sasa inauzwa Sh. 500,000.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema nchi itatumia fursa ya mkutano huo kujitafutia fursa za masomo na fedha za kuendeleza sekta ya kilimo na mifugo kwa kuwa Tanzania ni mzalishaji na muuzaji wa bidhaa za kilimo ndani na nje ya nchi.

Alisema baadhi ya wageni wameshawasili nchini na wanatembelea maeneo mbalimbali ya uwekezaji. Baada ya mkutano huu, kutakuwa na ongezeko la wawekezaji na kunufaisha Watanzania kitaalamu na kiteknolojia.

Aliwataka wadau wa zao la vanilla kupuuza taarifa kuwa zao hilo linaizwa Sh. milioni 1.5 kwa kilo kwa kuwa siyo za kweli zinalenga kupotosha jamii.

Alisema serikali inakiwanda kidogo cha kuchakata vanila mkoani Kilimanjaro na ina mpango wa kuweka kituo kingine kama hicho mkoani Kagera, ili kuwaondolea usumbufu wa madalali wakulima mkoani humo.

Pia alisema serikali inaandaa mikakati ili wakulima wa zao hilo na kahawa kulima kwa mkataba na hivi karibuni watatoa mwongozo kama ilivyo kwenye zao la parachichi.

Kuhusu alizeti, Bashe alisema serikali inaendelea kutoa mbegu bora kwa ruzuku na katika msimu wa kilimo wa 2022/23 wamegawa zaidi ya tani 1,000 kwa wakulima wa Singida na Dodoma ili kufikia uzalishaji wa tani milioni tatu katika kipindi cha miaka mitano.

Alisema serikali pia inachukua hatua mbalimbali za kutatua migogoro ya wakulima na wafugaji ambayo mengi inatokana na uhaba wa malisho na maji na kuwa mwaka huu inajenga mabwawa ya maji 100 kwa ajili ya kunyweshea mifugo.

Alisema Tanzania imepiga hatua kubwa katika uzalishaji wa mazao ya chakula kutoka tani milioni 18 mwaka 2020/21 mpaka tani milioni 20 mwaka 2022/23, hivyo kuwa na mweleleo mzuri kulifikia malengo kukua kwa sekta ya kilimo kwa asilimia 10 kufikia mwaka 2030.

## Tundu Lissu aibua hoja nzito kuporomoka bei ya pamba

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Bara, Tundu Lissu, amesema kuporomoka kwa bei ya pamba kutoka Sh. 2,200 hadi 1,060 kwa kilo msimu huu kumetokana na sekta hiyo kushikiliwa na viongozi wenye maslahi binafsi na wafanyabiashara wanaoendelea kuhodhi soko la zao hilo.

Kiongozi huyo wa kisiasa alitoa kauli hiyo juzi mkoani Simiyu wakati wa mwendelezo wa ziara yake pamoja na viongozi wengine wanaoendesha wanachokiita 'Operesheni +255 Katiba Mpya Okoa Bandari Zetu'.

Operesheni hiyo inaendelea katika Kanda ya Serengeti, Lissu akishauri kuchukuliwa hatua kali dhidi ya watumishi wanaojihusisha na biashara hiyo.

Alitaja sababu ya kushuka kwa bei hiyo ni mgongano wa kimaslahi walionao watumishi hao, wakitaka kununua pamba kwa bei ya chini kisha waiuze kwa bei kubwa kinyume cha Sheria ya Utumishi wa Umma, inayowazuia kujihusisha na biashara.

"Tatizo linaanzia kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Pamba. Ni mfanyabiashara wa zao hilo, viongozi wa maeneo mbalimbali ambao ndio wanaopanga bei ya pamba, wote ni wafanyabiashara wa zao hilo ambako kwa hali isiyo ya kawaida wanapambana kushusha bei ya zao ili waiuze kwa bei kubwa na kupata faida ya juu," alidai.

Lissu alitaja kushuka kwa bei ya pamba ni mkakati wa makusudi ili kuwanufaisha watu wachache wanaojihusisha na bisashara hiyo wakiwa katika utumishi wa umma kinyume cha utaratibu. Wanaumiza wakulima.

"Sasa ninyi shauri zenu. Kwa hali hii, mtaendelea kunyanyasika na nguvu zenu kutumika kuwanufaisha wengine msipokubali kubadilika. Na mimi siwezi kufanya mabadiliko haya mwenyewe bila ninyi," Lissu alisema.

**BASHE AMJIBU**

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, akizungumza na wahariri wa vyombo vya habari katika mkutano ulioandaliwa na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu, jijini Dar es Salaam jana, alikanusha madai hayo ya Lissu. Bashe aliyaita ni madai ya uongo. Serikali itapita kila eneo ambalo wametoa taarifa hizo kwa ajili ya kufafanua.

Waziri huyo alifafanua kuwa bei hiyo ya pamba ni ya ulimwengu mzima; wastani bei ya zao hilo duniani wakati Tanzania inauzwa Sh. 2,000 katika soko la dunia ilikuwa ni wastani wa Sh. 3,019 (Dola 1.2) mpaka Sh. 3,164 (dola 1.3) kwa kilo.

"Nimemsikia kiongozi mmoja anasema bei ya pamba imeshuka kisa wabunge, viongozi wa Bodi ya Pamba ni wafanyabiashara wa zao hilo.

"Ameeleza kuwa ni kinyume na maadili ya uongozi, lakini anasahau kuwa mwenyekiti wake (akimlenga Freeman Mbowe) alikuwa mfanyabiashara na alikuwa mbunge kwa kipindi hicho," Bashe alisema.

Waziri huyo aliendelea kufafanua kuwa kwa nchi zinazouza kwa bei ya Sh. 900 mpaka 1,000, mkulima wa pamba anajinunulia mbegu pamoja na dawa mwenyewe, tofauti na mkulima wa Tanzania ambaye anapewa ruzuku ya mbegu na pembejeo, hivyo bei ya pamba iliyoko sokoni mkulima anaichukua fedha kama ilivyo bila makato.

"Hoja ya mkulima siyo kwamba bei ya pamba ni shilingi ngapi, bali ni matumizi ya gharama kiasi gani katika kuzalisha zao hilo mpaka anafikia mavuno yake na amepata faida kiasi gani,"alisema Bashe.

**ULINZI RASILIMALI**

Wakati Lissu na Bashe wakitoa kauli hiyo, Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, ameendelea kukumbusha wananchi kuhakikisha wanashiriki kikamilifu katika kulinda na kusimamia rasilimali za taifa na kutokubaliana na alichokiita udanganyifu kuhusu mali zao na vizazi vyao vya baadaye.

Akiendelea na mikutano ya operesheni hiyo mkoani Mara katika Jimbo la Mwibara. Mbowe aliwataka wananchi kushiriki kulinda rasilimali za nchi yao badala ya kuacha jukumu hilo kwa wanasiasa.

## HABARI KITAIFA

# Jela miaka 30 kwa kusafirisha bangi

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Morogoro imemhukumu Awadhi Mohamed, kwenda jela miaka 30 kwa kosa la kusafirisha bangi yenye uzito wa kilo 34.65.

Hukumu hiyo imetolewa mwishoni mwa wiki na Hakimu Mkazi Mkuu, Livini Lykinana baada ya kuridhika na ushahidi wa pande zote mbili.

Katika shauri hilo upande wa Jamhuri uliwakilishwa na Wakili wa Serikali, Elias Masini na ulikuwa na jumla ya mashahidi watano, mshtakiwa alijitetea mwenyewe.

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu Lyakinana alisema mahakama inatoa adhabu hiyo kwa mujibu wa sheria na pia iwe fundisho kwa wote wanaojihusisha na biashara ya dawa za kulevya.

Baada ya mshtakiwa kutiwa hatiani aliomba mahakama impunguzie adhabu kwa madai kuwa ni mara yake ya kwanza kutenda kosa la jinai, familia yake inamtegemea na pia ana matatizo ya uti wa mgongo.

Mshtakiwa alikamatwa na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Desemba 22, 2022 katika kijiji cha Chogoali Sokoni Kata ya Iyongwe, Wilaya ya Gairo mkoani Morogoro akiwa na kilo 34.64 za dawa za bangi alizokuwa ameficha na kuzihifadhi katika mifuko ya sandarusi.




Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo, akizungumza na wafanyabiashara wa Soko la Kariakoo katika Mkutano wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Kariakoo (JWK). Kushoto ni Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo, Martin Mbwana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Wasiojulikana wavunja kanisa, waiba sakramenti

**Na Vitus Audax**

WATU wasiojulikana wanadaiwa kuvuja na kuingia katika Kanisa la Mt. Bernadetha wa Lurdi Parokia ya Nyakato-Buzirayombo na kuvunja eneo la kutunza Ekaristi Takatifu 'Tabernakulo' kisha kuzitupa na nyingine kuondoka nazo.

Tukio kama hilo ni la pili kutokea ndani ya mwaka huu, la kwanza lililotokea katika Jimbo Katoliki la Geita.

Kutokana na kitendo hicho, uongozi wa kanisa hilo umeamua kulifungakwa mujibu wa sheria za kanisa kanuni namba 1211-1213.

Taarifa iliyotolewa jana na Makamu wa Askofu wa Jimbo Katoliki la Rulenge Ngara, Fr. Ovan Mwenge, ilisema kuwa tukio hilo lilitendeka usiku wa kumkia Septemba Mosi, huku waliohusika na kitendo hicho hawajafahamika mpaka sasa.

Taarifa hiyo ilisema mtu/watu hao waliingia kanisani humo kwa kuvunja ukuta na kisha kuvunja Tabernakulo ambamo Ekaristi Takatifu uhifadhiwa na kufanya kufuru kwa Sakramenti hiyo kwa kuila ama kuondoka nayo na nyingine kuitelekeza sakafuni ndani na nje ya kanisa hilo.

"Uharibifu huu ni kufuru kwa sakramenti na umelinajisi kanisa kuu na Parokia ya Nyakato-Buzirayombo.

Pia umeathiri kwa kiasi kikubwa utakatifu wa kanisa la parokia, hivyo kuvunja adhi na heshima ya waamini na jamii kwa ujumla," ilisisitiza taarifa hiyo.

Vile vile, taarifa ilisema kutokana na tukio hilo na kadiri ya maelekezo ya sheria za kanisa, kanuni namba 1211-1213 na kwa maelekezo ya Askofu Severine NiweMugizi, ametangaza kufungwa kwa kanisa hilo kwa muda wa siku 30 kuanzia Septemba 2, mwaka huu.

Taarifa imefafanua kuwa yatafanyika marekebisho na ukarabati na baadaye litabarikiwa na kutakaswa ili liendelee kutumika na katika kipindi hicho cha kurekebishwa waamini katika Jimbo la Rulenge watatakiwa kusali na kufunga, kufanya toba na malipizi kwa Mwenyezi Mungu ili kubadilisha mioyo ya watu wenye nia ovu kwa mambo matakatifu.

# Wapendekeza kifungo cha maisha kilegezwe

**Na Halfani Chusi**

BAADHI ya wakazi mkoani Lindi, wamependekeza maboresho ya sheria za haki jinai nchini ikiwamo mtu anapofanya kosa la mauaji asihukumiwe kunyongwa bali apewe adhabu kubwa kama kifungo cha miaka 70 hadi 90 gerezani.

Walitoa maoni yao mbele ya wajumbe wa Tume ya Haki Jinai, kuwa kumekuwa na uonevu unaofanyika katika mnyororo huo ambao utamalizwa kwa marekebisho ya sheria na muundo.

Akitoa maoni yake, Mohamedi Mbuta alisema kuwapo kwa kifungo cha maisha haijawa suluhisho la matukio ya jinai kwenye jamii na kwamba ni muhimu kuweka ukomo.

Debora Charles, alisema mfungwa anayekaa gerezani mpaka anazeeka na kushindwa kutembea iangaliwe namna ya kumruhusu arudi uraiani kwa sababu unakuwa mzigo kwa wenzake.

Mwananchi mwingine, Omeni Makwita, alilalamikia kitendo cha mahakama kuwataka watu kufikisha malalamiko yao kwa kutumia lugha ya Kiingereza akidai wengi hawajasoma na hawajui lugha hiyo vizuri na kwamba suala hilo linanyima haki.

Athumani Mtengeleka, alishauri ukamataji wa mtuhumiwa hasa mtoto, ufuate sheria akiliomba Jeshi la Polisi, kujiepusha na kumnyooshea silaha mtoto mdogo kitendo kinachokiuka sheria na haki. "Askari polisi anamkamata mtuhumiwa bila kujitambulisha, wanapaswa kujua kwamba kila mtu hana hatia mpaka mahakama itakapo thibitisha," alisema.

Mjumbe wa Tume hiyo, Prof. Edward Hosea, aliyataja mambo yaliyobainika wakati wa ukusanyaji wa taarifa zao kwa wananchi kuwa vyombo vya ulinzi vimekuwa haviwajibiki kuzuia uhalifu bali vikikamata watuhumiwa bila kuwafanyia uchunguzi na kuwafikisha mahakamani jambo linalosababisha kuwa na mrundikano wa mahabusu wengi na wasio na hatia.

Alisema jambo jingine ni kutokuwa na mkakati maalumu wa kitaifa wa kubaini na kuzuia uhalifu na kwamba tume hiyo inapendekeza serikali ishirikiane na wadau wengine ili kuja na mkakati wa kuzuia na kubaini wahalifu.

Alisema maeneo mengi wananchi walipendekeza kurejeshwa mfumo wa nyumba kumi kwa sababu ni rahisi kubaini uhalifu katika nyumba kumi kama ilivyo sasa wadau wakubali turejee katika mfumo tuige mfano wa Zanzibar. Mapendekezo mengine ni huduma za kijamii na kibiashara zifungamanishwe na mfumo wa usajili kila mtu awe na namba moja tu akisisitiza mfumo huo utafanywa na watu wote tuwe na kitambulisho kimoja.

"Vyombo vya haki jinai, mamlaka ya kukamata vitekeleze majukumu yao kwa kushirikisha na Jeshi la Polisi na libaki na mtuhumiwa kama umekamatwa na taasisi ya kuzuia na kupambana na rushwa basi upelekwe mahabusu ya polisi na sio sehemu nyingine," alishauri Prof. Hosea.

# TCD yataka 'viraka' Katiba ya 1977 vizibwe kabla ya uchaguzi 2024/25

**Na Halfani Chusi**

KITUO cha Demokrasia Tanzania (TCD), kimeishauri serikali kufanya mabadiliko madogo katika Katiba ya sasa ili kuwa na Tume huru ya Uchaguzi itakayowezesha Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2024 na Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 kufanyika kwa uhuru, haki na ushiriki mpana wa demokrasia.

Kituo hicho kimetoa ushauri huo baada ya kubaini serikali imechelewa kuanzisha mchakato wa upatikanaji Katiba Mpya na kuna uwezekano isipatikane kabla ya uchaguzi huo.

Mwenyekiti wa kituo hicho, Prof. Ibrahimu Lipumba, aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salama, alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu maazimio ya mkutano wa wadau wa kitaifa kujadili hali ya demokrasia nchini kuelekea uchaguzi wa 2024-25 uliofanyika kwa siku mbili mfululizo Agosti 22 na 23 mwaka huu.

Kiongozi huyo ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi (CUF), aliyataja maazimio hayo kuwa ni pamoja na Serikali kukubali misaada ya kuimarisha utendaji wa tume kutoka kwa washirika wa maendeleo kama vile UNDP na wengine.

"Vyama vya siasa Zanzibar, viendeleze utashi wa kisiasa katika utekelezaji wa kudumisha dhana ya maridhiano kuelekea Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025, uchaguzi wa Zanzibar ufanyike kwa siku moja ili wadau wa demokrasia waweze kuandaa mkutano wa hali ya demokrasia kwa upande wa Zanzibar ili kudumisha dhana ya maridhiano na utatuzi wa changamoto kwa pamoja.

"Pia, serikali iwezeshe na kusaidia majadiliano baina ya vyama vya siasa, asasi za kiraia na mashirika ya kiserikali ili kuhakikisha kunakuwa na mtazamo wa pamoja katika kujenga dhana ya ushirikiano kushinda kwa hoja bila kupingwa," alisema.

Prof. Lipumba aliyataja maazimio mengine ni kuwekeza uhuru wa kutoa maoni na kujieleza kwa wananchi, viongozi vyama vya siasa na asasi za kiraia, vyama vya siasa viwe na kanuni zinazoelezea na kuongoza mchakato wa uteuzi wa wagombea wa nafasi za viti maalum vya wanawake zinazoakisi misingi ya uwazi, usawa na demokrasia.

"Fedha zilizotengwa na serikali kwa ajili ya elimu kuhusu Katiba ya mwaka 1977, zipelekwe kwa asasi za kiraia na elimu hii iwe endelevu katika mchakato mzima wa mabadiliko ya katiba, taarifa ya Jaji (Joseph) Warioba na viambatanisho vyake hususani randama, zitumiwe katika elimu kuhusu katiba.

"Pia ninashauri, muswada wa mabadiliko ya katiba upelekwe pamoja na muswada wa Tume huru ya Uchaguzi katika mkutano ujao wa Bunge kama ilivyofanyika mwaka 1992 wakati wa kuridhia mfumo wa vyama vingi.

"Muda uliobakia kuelekea uchaguzi ni mfupi. Mkutano wa kitaifa wa maridhiano uliofanyika Aprili 2022 Dodoma, ulijadili na kuwasilisha serikalini muswada wa mfumo wa sheria ya uchaguzi huru na wa haki," alisema.

Mkutano huo uliokutanisha vyama vyote vya siasa vyenye usajili wa kudumu nchini, ulifanyika Agosti 22 na 23 mwaka huu.



Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji Mkoa wa Pwani, Nctobere Msamau, akizungumza kwenye mkutano mkuu wa halmashauri kuu wa chama cha wafugaji kuhusu kujadili na kutatua migogoro kati ya wafugaji na serikali uliofanyika Dodoma juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Majaliwa: Tutaendelea kuheshimu mchango wa madhehebu ya dini

**Na Mwandishi Wetu,** TANGA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali itaendelea kuthamini, kutambua na kuheshimu mchango wa madhehebu ya dini katika kuimarisha utoaji na upatikanaji huduma bora za jamii kwa wananchi.

Aliyasema hayo jana alipomwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan katika ibada ya kuwekwa wakfu na kusimikwa kwa Askofu Mteule Thomas Kiangio, Askofu wa Jimbo la Tanga, iliyofanyika Kanisa Kuu la Mtakatifu Antony wa Padua lililoko Chumbageni, jijini Tanga.

Waziri Mkuu alitoa rai kwa viongozi wa dini, waamini na Watanzania kwa ujumla wazidishe upendo, umoja na mshikamano kwa sababu asili ya dini ni upendo kwa Mungu na kwa mwanandamu.

"Hivyo basi, uwapo wa upendo ni msingi mzuri wa kuendelea kulinda amani tuliyonayo katika Taifa letu.

"Hata leo tumeshiriki kwenye misa hii kwa utulivu kabisa kutokana na amani iliyopo. Sina shaka kuwa mtakubaliana nami kuwa Watanzania wote ni wacha Mungu, wanaotii sheria za Mungu na zile za serikali na wanatambua wajibu wao wa kiroho wa kutii mamlaka zilizopo," alisema.

Waziri Mkuu alisema Rais Samia ni kinara katika suala la maridhiano, akifafanua: "Tunayo bahati ya kuwa na serikali inayosikiliza, inayosimamia haki, uhuru, misingi ya demokrasia na utawala bora wa sheria.

"Tumeona dhamira njema ya Mheshimiwa Rais, kwa kutenga muda wa kukutana na makundi mbalimbali ikiwamo Baraza la Maaskofu. Nitoe wito kwetu sote kutumia uhuru tuliopewa, lakini tukizingatia mipaka ili kuendelea kudumisha amani na demokrasia nchini."

Waziri Mkuu pia alitumia fursa hiyo kuwashukuru viongozi wa madhehebu ya dini kwa kuunga mkono serikali katika kutoa huduma kwa jamii ya Watanzania kwa kuwa wamekuwa wanawasaidia watu wenye uhitaji, wamekuwa walezi kwa vijana na yatima na kutoa huduma kwa wagonjwa, tena bila kujali tofauti za kiimani.

Majaliwa alisema uhusiano kati ya serikali na madhehebu ya dini umekua kutokana na dhamira ya dhati ya serikali ya kuendelea kushirikiana na dini zote katika kukuza ustawi wa wananchi kijamii na kiuchumi.

"Ushirikiano uliopo katika ya madhehebu ya dini na serikali umechagiza katika kuimarisha maisha ya Mtanzania mmoja mmoja na taifa kwa ujumla," alisema.

Askofu Kiangio alizaliwa tarehe 17 Machi 1965 katika Kijiji cha Mazinde Ngua wilayani Korogwe, Tanga. Anakuwa askofu wa tano baada ya kifo cha aliyekuwa Askofu wa Jimbo Katoliki la Tanga, Askofu Anthony Banzi, aliyefariki dunia tarehe 20 Desemba 2020.

# Wakufunzi vituo vya NBAA waitwa mabadiliko mitaala

**Na Getrude Mbago**

BODI ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu Tanzania (NBAA) imeendesha warsha kwa njia ya mtandao kwa wakufunzi wa vituo vya kufundishia wanafunzi wanaotarajia kufanya mitihani ya bodi ili kuwaongezea ujuzi.

Katika ufunguzi wa warsha hiyo jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa bodi hiyo, Pius Maneno, alisema lengo la warsha hiyo ni kuwakumbusha majukumu yao ili kuendana na mitaala wa bodi.

Maneno alisema mafunzo ya wakufunzi wa vituo vya kufundishia mwaka huu yamekuja na mabadiliko ya mitaala ya masomo ya bodi, hivyo amewataka kujadili vyema ili wanapokwenda kutoa elimu, wawe na uelewa mzuri.

Aliongeza kuwa lengo kubwa la NBAA ni kuona wanapandisha kiwango cha ufaulu kwa mitihani mbalimbali pamoja na kuongeza kiwango cha uelewa ili kipindi wanapomaliza mitihani yao wawe wabobezi kwenye masuala ya uhasibu na u7kaguzi.

Pia aliwataka wakufunzi wa vituo vya kufundishia masomo ya bodi kuendesha masomo kwa njia ya mtandao ili kupunguza gharama za uendeshaji, kuwafikia wanafunzi wengi na kuendana na teknolojia.

Meneja wa Idara ya Elimu na Mafunzo NBAA, Peter Lyimo, alisema bodi imejipanga vizuri ili kuhakikisha kila mtahiniwa anafanya mitihani vizuri na kuhakiksiha wanaondoa changamoto zote.

# Bil 1/- kuwezesha utafiti

**Na Renatha Msungu**

SERIKALI kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, imetoa Sh. bilioni moja kwa taasisi na watafiti waliokidhi vigezo vya kufanya utafiti katika sekta za elimu, kilimo, afya na uvuvi.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Prof. Carolyne Nombo, ameagiza fedha hizo zitolewe haraka ili watafiti hao waanze kufanya utafiti wao mapema na kutatua changamoto za kijamii.

Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Dk. Amosi Nungu, katika hafla ya ufungaji wa mafunzo ya siku tatu kwa watafiti wanufaika wa mradi huo mkoani Dar es Salaam wiki iliyopita, alisema mchakato wa kupata washindi hao ulihusisha watafiti 92 walioomba kufanya utafiti.

Alisema kuwa baada ya mapitio ya awali, watafiti 57 walikidhi vigezo vya kupelekwa kwa wataalamu na baadaye miradi saba ilichaguliwa kwa kuzingatia ufaulu wa juu zaidi.

"Ilikuwa kazi ngumu sana kuwapata watafiti hawa na wanakwenda kushirikiana na sekta binafsi ili kuhakikisha wanafanikisha kufanya utafiti huo," alisema Dk. Nungu. Alisema kila taasisi na mshindi wake watakabidhiwa Sh. milioni 150 kwa ajili ya kukamilisha utafiti waliomba, huku akisisitiza kila mtafiti na taasisi yake wanapaswa kuzingatia vigezo na masharti katika fedha walizokabidhiwa.

Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Ufundi, Prof. Nombo, alisema fedha hizo zinapaswa kutolewa kwa wakati kwa wahusika ili waende kufanya utafiti ambao utaleta matokeo chanya kwa jamii.

"Ninawapongeza sana COSTECH kwa kazi nzuri mnayoifanya. Ninaomba hizi fedha zitolewe kwa wakati kwa wahusika ili wakafanye kazi yao kwa weledi na kuwanufaisha wananchi," aliagiza.

Manyama Venance, Ofisa wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), alisema washirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na wamekuja na utafiti wa kutumia akili bandia kuongeza uwazi na uwajibikaji katika mifumo ya ununuzi na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo.

"Kumekuwa na tatizo kubwa la rushwa na ubadhirifu wa fedha za maendeleo na utafiti umeonesha fedha nyingi zinapotea katika mchakato wa ununuzi," alisema Venance.

Alisema utafiti huo wa kutumia akili bandia, utaiwezesha TAKUKURU kubaini viashiria vya rushwa katika maeneo mbalimbali wakati mchakato wa ununuzi unaendelea.

# MATANGAZO



## POSITIONS ANNOUNCEMENT

### RESEARCH TECHNICIAN – TWO POSITIONS

**IITA-TZ-2023-NRS-014-NRS-DSM**

The International Institute of Tropical Agriculture (IITA) is a not-for-profit institution that generates agricultural innovations to meet Africa's most pressing challenges of hunger, malnutrition, poverty, and natural resource degradation. Working with various partners across sub-Saharan Africa, we improve livelihoods, enhance food and nutrition security, increase employment, and preserve natural resource integrity. IITA is a member of CGIAR, a global agriculture research partnership for a food secure future.

IITA is looking for a suitably qualified person to fill the positions of Research Technician to support the IITA banana project based at the IITA Office at the Nelson Mandela African Institution of Science and Technology (NMAIST) in Kijenge, Arusha.

**Responsibilities:**

- Collection of data from field, screenhouse and lab experiments.
- Uploading of data using digital platforms.
- Assisting with other breeding operations in the field, screenhouses, and lab as directed by the supervisor.
- Routine maintenance of screen- house and on station experimental sites.
- Provides assistance to student projects.
- Supervision and coordination of screen house and field casual labour.
- Assist the data collection manager in germplasm management.
- Assisting in report preparation upon request.

**Required Qualifications / Experience**

- BSc in Agricultural studies with at least 2 years' experience.
- Ability to work independently with minimal supervision, but also participate as a team member in accomplishment of duties.
- Experience in scientific data collection.
- Possess excellent interpersonal and communication skills in English.
- The ability to work independently.

The initial contract for the position is for one year: renewable subject to performance and availability of funds. The duty station for the position will be IITA in Arusha. This is a nationally recruited position and IITA offers a competitive remuneration package.

**Applications:** Applications including curriculum vitae, copies of certificates, telephone number, email address, and names and addresses of two referees should be sent to the Country Representative, IITA-Tanzania, Plot No. 25, Mwenge – Coca-Cola Road, Mikocheni Industrial Area P.O. Box 34441, Dar es Salaam, Tanzania or by email to **IITA-Tanzania@cgiar.org**

Applicants are requested to please indicate the reference number for the position as indicated on the heading of the announcement in your application as well as on the subject of your email if sending by email. If sending by post or hand delivery, please indicate the reference number on your application as well as on the left-hand side of your envelope.

Please note that any applications without the reference indicated will be automatically disqualified.

**Closing date:** Two weeks from the date of advertisement appearing in the newspaper. Please note that only shortlisted candidates will be contacted.

217582401

## POSITIONS ANNOUNCEMENT

### DATA COLLECTION MANAGER

**IITA-TZ-2023-NRS-013-NRS-DSM**

The International Institute of Tropical Agriculture (IITA) is a not-for-profit institution that generates agricultural innovations to meet Africa's most pressing challenges of hunger, malnutrition, poverty, and natural resource degradation. Working with various partners across sub-Saharan Africa, we improve livelihoods, enhance food and nutrition security, increase employment, and preserve natural resource integrity. IITA is a member of CGIAR, a global agriculture research partnership for a food secure future.

IITA is looking for a suitably qualified person to fill the position of Data Collection Manager to support the IITA banana project based at the IITA Office, at the Nelson Mandela African Institution of Science and Technology (NMAIST) in Kijenge, Arusha.

**Responsibilities:**

- Plans experiments and ensures quality and accurate data is collected and uploaded into the databases.
- Interfaces with other disciplines to ensure that all breeding related data is uploaded onto the database following appropriate protocols.
- Supervises data collection staff.
- Assumes responsibilities of post-doc breeder when breeder is absent from station.
- Keeps good custody and maintenance of data collection gadgets and apps (including charges)
- Identifies and reports on needs for updating, upgrading, or replacing the data collection equipment.
- Assist with initial statistical analysis and report writing.
- Serves as first contact with those responsible for database and related programs.

**Required Qualifications / Experience**

- MSc in breeding, statistics or related fields preferred more than 3 years' experience.
- Experience in experimental design and statistical analysis and has profession in using modern analytical tools.
- Possess excellent interpersonal and communication skills in English.
- Demonstrated ability to write quality technical reports.
- Programing skills preferred.
- Experience in banana research is an added advantage.
- Ability to work independently with minimal supervision, but also participate as a team member in accomplishment of duties.

The initial contract for the position is for one year: renewable subject to performance and availability of funds. The duty station for the position will be IITA in Arusha. This is a nationally recruited position and IITA offers a competitive remuneration package.

**Applications:** Applications including curriculum vitae, copies of certificates, telephone number, email address, and names and addresses of two referees should be sent to the Country Representative, IITA-Tanzania, Plot No. 25, Mwenge – Coca-Cola Road, Mikocheni Industrial Area P.O. Box 34441, Dar es Salaam, Tanzania or by email to **IITA-Tanzania@cgiar.org**

Applicants are requested to please indicate the reference number for the position as indicated on the heading of the announcement in your application as well as on the subject of your email if sending by email. If sending by post or hand delivery, please indicate the reference number on your application as well as on the left-hand side of your envelope. Please note that any applications without the reference indicated will be automatically disqualified.

**Closing date:** Two weeks from the date of advertisement appearing in the newspaper. Please note that only shortlisted candidates will be contacted.

217582401

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kipenga AFL kimepulizwa, Simba jipangeni mapema

**KIPENGA** cha kuanza michuano ya klabu nane bora barani Afrika, African Football League (AFL), kimepulizwa mwishoni mwa juma baada ya droo ya mashindano hayo kufanyika Jumamosi.

Katika droo hiyo iliyofanyika jijini Cairo, Misri, Simba ambayo ni mwakilishi pekee wa Ukanda wa Afrika Mashariki (Cecafa), imepangwa kufungua michuano hiyo dhidi ya Al Ahly ya Misri, Oktoba 20, mechi itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, kabla ya timu hizo kurudiana nchini Misri Oktoba 24, mwaka huu.

Mshindi wa jumla wa mechi hiyo ya Simba dhidi ya Al Ahly, atakutana nusu fainali na mshindi wa jumla dhidi ya Petro de Luanda ya Angola na Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini ili kupata timu itakayotinga fainali.

Katika droo hiyo, TP Mazembe ya DR Congo yenyewe itavaana na Esperance ya Tunisia ambapo mshindi wa jumla wa mechi hiyo atacheza nusu fainali dhidi ya mshindi kati ya Enyimba na Wydad Casablanca ya Morocco ili kupata mwanafainali mwingine.

Hivyo, maandalizi makubwa kwa wawakilishi wetu hao, Simba, yanapaswa kufanyika ili kwenda kulitangaza vema soka la Ukanda wa Cecafa kwa ujumla, lakini kutotia aibu katika mechi hiyo ya ufunguzi ambayo itahudhuriwa na viongozi wakubwa wa soka duniani, akiwamo Rais wa Fifa, Gianni Infantino pamoja wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF), Patrice Motsepe.

Uwapo wa viongozi hao wa soka ambao wanatarajiwa kuambatana na wachezaji nguli wa soka duniani, ni wazi ulimwengu wa soka utaitupia jicho mechi hiyo ya ufunguzi, jambo ambalo Simba inatakiwa kufanya maandalizi makubwa ili kuionesha dunia kwamba Tanzania na Ukanda wa Cecafa kwa ujumla kuna vipaji vikubwa.

Tunaamini usajili Simba ilioufanya ni wa kiwango cha juu, hivyo kinachohitajika kwa sasa nikuendelea kufanya maandalizi ya kimbinu pamoja na kupata mechi nyingi za kimataifa za kujipima uwezo. Hatuna shaka pia na benchi la ufundi la Simba chini ya Mbrazili Robertinho Oliveira, hivyo ni suala la uongozi kulipa ushirikiano mkubwa kwa kila linachohitaji katika maandalizi yao hususan kupata mechi kubwa za kujipima uwezo.

Lakini pia ni wakati wa kila mchezaji katika kikosi hicho, kutambua na kuona umuhimu mkubwa wakufanya maandalizi binafsi kuelekea mechi hiyo ambayo tunaamini pia itakuwa ni daraja kwao kutangaza vipaji vyao.


Tunasema hivyo kutokana na kuwa na ushahidi wa kutosha kwa wachezaji wengi kunufaika na michuano mikubwa kama hiyo kwa kupata timu kubwa nje ya Tanzania kwenda kucheza soka la kulipwa kwa maslahi makubwa zaidi.

Mfano mzuri na wa hivi karibuni ni viungo washambuliaji wa Simba, Luis Miquissone na Clatous Chama, ambao kupitia michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika 2021, walionesha kiwango kikubwa katika hatua ya makundi hususan dhidi ya Al Ahly na msimu uliofuatwa kusajiliwa na klabu kubwa Afrika.

Miquissone alisajiliwa na Al Ahly huku Chama akisajiliwa na RS Berkane ya Morocco, kabla ya wawili hao kurejea tena Simba baada ya mambo kutowaendea vizuri katika klabu hizo.

Hivyo, pamoja na kutaka kuisaidia klabu yao, lakini kila mchezaji anapaswa kutambua hilo ni daraja sahihi kwake kuonyesha uwezo binafsi na kitimu kwani wakishinda na kutinga nusu fainali na kisha fainali, ndivyo wanavyojitangaza zaidi duniani. Hivyo, tunaitakia klabu hiyo maandalizi mema huku ikitambua Watanzania na Wanaafrika Mashariki wote wapo nyuma yao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Hongera JKT Queens, jipangeni ubingwa Afrika inawezekana

Na Adam Fungamwango

**KWA** misimu miwili mfululizo Tanzania imekuwa kinara kwenye soka la wanawake Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, maarufu CECAFA baada ya timu za Simba Queens na JKT Queens kuwa mabingwa.

Mwishoni mwa wiki, kikosi cha JKT Queens kikiwa nchini Uganda kilifanikiwa kutwaa Ubingwa wa Afrika Mashariki na Kati kwa kuifunga CBE ya Ethiopia kwa mikwaju ya penalti 5-3 baada ya kutoka suluhu.

JKT Queens imetwaa ubingwa huo bila kupoteza mechi yoyote ile na imeshinda mechi zote tangu makundi hadi fainali ndipo ilipotoka sare na kushinda kwa penalti. Kwa sasa wao ndiyo watakuwa wawakilishi wa Ukanda wa CECAFA kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika inayotarajiwa kuchezwa baadaye mwaka huu.

JKT Queens wanarudia kile ambacho Simba Queens ilikifanya msimu mmoja uliopita ilipotwaa ubingwa wa CECAFA kwa kuifunga She Corporate ya Uganda bao 1-0 mechi ikichezwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam, ikapata tiketi ya kwenda kuuwakilisha ukanda huu kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika na kushika nafasi ya nne.

Nichukue nafasi hii kuwapongeza wachezaji, benchi la ufundi, viongozi, Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), pamoja na Watanzania wote. Nilichokiona ni kwamba timu hiyo ilikuwa inacheza mechi moja baada ya nyingine kulingana na ubora wa timu inayocheza nayo hadi kufanikiwa kuwa mabingwa.

Pia nilichokiona ni aina fulani ya ushirikiano kati ya viongozi wa JKT Queens ambao hawakuwa wabinafsi, kwani walichukua pia baadhi ya watu wa benchi la ufundi la Twiga Stars na timu za chini za wanawake wakaongeza nguvu kwenda kuitetea nchi.

Ndiyo maana alikuwapo Kocha Mkuu wa timu za soka za Wanawake Tanzania, Bakari Shime, ambaye aliungana na Kocha wa timu hiyo, Ester Chabruma, kwa ajili ya kuongeza mbinu na maarifa kwa manufaa ya taifa.

Shime akapewa cheo cha Mkurugenzi wa Ufundi, lakini lengo likiwa ni lile lile ashirikiane na Chabruma na kwa kiasi kikubwa ilileta umoja kwani asilimia kubwa ya wachezaji wa JKT Queens pia ni wachezaji wa timu za soka za wanawake kwa umri mbalimbali.

Kwa maana hiyo wachezaji hawakuwa na ugeni kwa mkurugenzi huyo wa ufundi.

"Kwa sasa tumepata nafasi ya kuuwakilisha Ukanda wa CECAFA kwenye Ligi ya Mabingwa, tutarudi kukaa chini kuangalia pale ambapo tuliteteleka tuparekebishe ili tukienda tuvuke pale timu ya Tanzania, Simba Queens ilifika msimu uliopita," anasema Shime.

Kinachotakiwa kufanya ni marekebisho na kuangalia ni kitu gani ambacho kiliwafanya Simba Queens msimu uliopita kushindwa kushika nafasi ya tatu au kutinga fainali achilia mbali kutwaa ubingwa.

Kushika nafasi ya tatu tu kwa JKT Queens kutaweza kuivunja rekodi ya Simba Queens, hivyo juhudi za dhati zinatakiwa kufanyika ili kuweza kufanikisha hilo.

Ushirikiano na mshikamano ulioonyeshwa kwenye michuano ya CECAFA unatakiwa kuendelea pia kwenye maandalizi na Ligi ya Mabingwa Afrika.

Napenda kuziuma sikio klabu za soka wanawake nchini kuwa iwapo zitaongeza kidogo tu uwekezaji kwa kusajili wachezaji bora, inawezekana kabisa isipite miaka hata mitano kabla ya timu yoyote hapa nchini kutwaa Ubingwa wa Afrika.

Tayari inaonyesha Tanzania imeshalishika na kuwa kinara kwa Ukanda wa CECAFA, hivyo kinachoonekana ni kukosa ubora kidogo wa baadhi ya wachezaji ili kuanza kuitawala Afrika kwa upande wa klabu.

Kilichoigharimu Simba msimu uliopita ni kwamba wachezaji wake walikutana na wenzao waliozidi viwango kidogo hivyo, JKT Queens kama itaongeza baadhi ya wachezaji wenye viwango vya juu kidogo inaweza kushangaza wengi kwa kurejea na kombe.

HABARI KITAIFA

# TPDC yazipa mtihani kampuni zake tanzu

**Na Gwamaka Alipipi**

MWENYEKITI wa Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Balozi Ombeni Sefue, ameziagiza bodi za kampuni tanzu za shirika hilo; TANOIL na GASCO kujiendesha kibiashara na kutoa gawio kubwa kwa serikali.

Pia ameziagiza kuandaliwa mpango mkakati utakaoonesha namna zitakavyojitegemea, kujiendesha pasi na kutegemea msaada, kuwa wabunifu, wathubutu na wajasiriamali wa kweli, watakaoshindana na sekta binafsi.

Alitoa maagizo hayo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam alipozindua bodi za kampuni hizo tanzu za TPDC.

Hafla hiyo ilihudhuriwa pia na wawakilishi wa Ofisi ya Msajili wa Hazina, wajumbe wa Bodi ya TPDC pamoja na menejimenti za GASCO na TANOIL.

"Hatimaye tumeshuhudia uzinduzi wa bodi za kiutendaji za kampuni tanzu za TPDC ambazo ni TANOIL na GASCO. Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi ya TPDC, tunawapongeza mlioteuliwa kuingia katika historia ya kuwa kama bodi anzilishi. Mna wajibu mkubwa kuhakikisha historia hiyo inatukuka, siyo vinginevyo," alisema.

Balozi Sefue alisema TPDC ina jukumu kubwa la kusimamia maslahi ya serikali katika sekta ya mafuta, gesi asilia na kujiendesha kiushindani ndani na nje ya nchi.

"Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi ya TPDC, tunamshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa uamuzi wake wa kukubali ombi letu la kuwa na uhuru zaidi wa kujiendesha kibiashara, kuna watu wanafikiri mashirika ya umma hayawezi kujiendesha kibiashara, kujiendesha kwa faida na kushindana. Dhana hiyo haina ukweli wowote," alisema.

Alizitaka bodi hizo kuhakikisha zinakuwa na ubunifu, uthubutu, ujasiriamali wa kweli utakaoshindana na sekta binafsi, kuwa wawajibikaji wa kutekeleza majukumu kwa kuzingatia sheria, miongozo, kanuni na weledi.

Alisema Ofisi ya Msajili Hazina imeiondoa TPDC katika ofisi zinazopata ruzuku ya serikali, hivyo bodi hizo zinapaswa kuanza kuandaa mpango mkakati utakaoonesha namna zitakavyojitegemea kujiendesha kibiashara na hatimaye kutoa gawio kwa serikali.

Mwakilishi kutoka Ofisi ya Msajili Hazina, Neema Msomba, alizitaka bodi hizo zielewe maono ya kampuni mama (TPDC), wayatafsiri na kuyatekeleza na kuwa na uhusiano mzuri wa kiutendaji.

Pia alizitaka kuzisaidia menejimenti kufikia malengo na kuzingatia mipaka iliyowekwa, kutumia mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika kutoa huduma.

Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Mussa Makame, alipongeza serikali kwa kuweka kipaumbele katika sekta hiyo.

Alisema TPDC ilianzishwa mwaka 1969 na ilianza shughuli mwaka 1973, huku kampuni tanzu ya GASCO ikianzishwa mwaka 1985 ikiwa na lengo la kuimarisha miundombinu ya gesi na mafuta.

Alisema TANOIL ilianzishwa mwaka 1999 kwa lengo la kushiriki katika biashara ya mafuta na bidhaa za mafuta nchini.

Mwenyekiti wa bodi hizo, Willium Chiume, aliahidi watafanya kazi kwa weledi na kwa uaminifu, ubunifu na kuendeleza azma ya TPDC ya kujiendesha kibiashara.




Mhasibu wa Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni jijini Dar es Salaam, Livia Mhagama, akisoma mapato na matumizi pamoja shughuli mbalimbali zilizofanywa na kituo hicho mwaka jana, katika kikao cha kutathmini mafanikio na changamoto, mwishoni mwa wiki. **PICHA: SABATO KASIKA**

# CHADEMA yapokea wanachama wapya 100 toka ACT, CCM, CUF

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo(CHADEMA) Kanda ya Kusini kimepokea wanachama wapya zaidi ya 100 katika Kijiji cha Mitesa, Kata ya Mitesa wilayani Masasi mkoani Mtwara.

Wanachama hao wapya wamejiunga na chama hicho baada ya kurejesha kadi za vyama walikokuwa vya ACT-Wazalendo, Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Chama cha Wananchi (CUF).

CHADEMA pia imefungua matawi mapya mawili katika kijiji hicho na kuendelea kutoa wito kwa wananchi wa vijiji vingine wilayani Masasi na wilaya zingine za mikoa ya kusini kuendelea kuwaunga mkono kwa kuwa wao ni chama ambacho kinalenga kutatua matatizo ya Watanzania, hasa maeneo ya vijijini.

Katika mkutano wa hadhara wilayani Masasi mwishoni mwa wiki, Katibu wa CHADEMA Kanda ya Kusini, General Kaduma, alisema wamewapokea wanachama hao kutokana ajenda za chama hicho zinazolenga kukomboa wananchi wa mikoa ya kusini ambao wanadai kwa muda mrefu wamesahaulika kimaendeleo.

Alisema wananchi wa mikoa hiyo wamekuwa wakulima wakubwa wa mazao ya biashara kama vile mbaazi, korosho na ufuta, lakini mazao hayo hayawanufaishi kutokana na kutokuwa na soko la uhakika.

Alisema katika mkutano ambao wameufanya katika Kijiji cha Mitesa, wamepokea wanachama wapya zaidi ya 100 ambao wameamua kurejesha kadi za vyama vyao na kujiunga na CHADEMA.

Katibu huyo aliitaja ni hatua itakayowaongozea nguvu kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwakani na Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025.

Kaduma alisema mikoa ya kusini bado iko nyuma kimaendeleo katika maeneo yote ya msingi kuanzia elimu na miuondombinu yake hadi barabara, hivyo wakazi wa maeneo hayo kushindwa kunufaika na keki ya taifa.

Kaduma alisema CHADEMA itawekeza katika elimu kwa kuwa inaamini elimu ndio msimgi kwa binadamu yeyote yule ambaye anahitaji maendeleo.

Alisisitiza wanachama wapya ambao wamejiunga na CHADEMA, wanapaswa kujiona na kujiamini wako salama katika chama hicho ambacho kwa muda mrefu kimekuwa na uchungu na wananchi. Kinapiga kelele kwa serikali ili kuwakumbuka waliosahaulika kimaendeleo. "Siasa ndio maendeleo, hivyo wananchi msitambua na kuona hili, basi mtaendeleo kuwa maskini. Mwaka 2025 tunakwenda kufanya Uchaguzi Mkuu wa viongozi ngazi ya urais na wabunge, ndio wakati kufanya uamuzi sahihi wa kuchagua watu ambao watawaletea maendeleo na kuachana na umaskini huu mlionao hivi sasa," alisema Kaduma.

Alisema wananchi wa Kijiji cha Mitesa wamekuwa wanajitoa kwa moyo kuchangia miradi ya maendeleo mbalimbali, lakini wameendelea kuwa nyuma kimaendeleo.

Mwenyekiti wa CHADEMA Mkoa wa Mtwara, Shabani Mbaruku, alisema mikoa ya kusini imeendelea kuwa na umaskini licha kuwa na zao kubwa la kibiashara - korosho - ambalo linaingizia fedha nyingi za kigeni nchini.

Alisema kutokana na mikoa hiyo kuwa na utajiri mkubwa wa mazao, hawakupaswa kuwa na hali ya umaskini, lakini hali hiyo inajitokeza kutokana na viongozi walioko madarakani kutowathamini wananchi wa mikoa ya kusini kwa muda mrefu.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti baada ya kurejesha kadi za vyama walikokuwa na kujiunga na CHADEMA, Musa Issa na Asha Bakari waliokuwa wanachama wa CCM, walidai wamechoshwa na sera za vyama vyao kwa kuwa katika kijiji chao cha Mitesa hawajaona maendeleo yoyote yaliyofanyika licha ya wananchi kujitoa kwa dhati kushiriki shughuli za serikali.

Selemani Hassani kutoka Kijiji cha Mitesa, alidai kijiji chao hakijapewa kipaumbele katika maendeleo kulinganisha na vijiji vingine vya wilayani Masasi.

Ni hali aliyoitaja inatokana na kuwapo mvutano wa kisiasa miongoni mwa viongozi wa kata na wilaya, hivyo wameamua kujiunga na CHADEMA baada ya kuridhishwa na sera za chama hicho.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



# Waziri Mkuu, kampuni kubwa za madini Korea Kusini wateta

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amekutana na ujumbe kutoka Korea Kusini uliojumuisha viongozi wa kampuni kubwa za madini yanayohusika na mnyororo wa thamani wa uzalishaji betri za magari za Posco Holdings, Posco International, SK, Korea Zinc na LX International.

Majaliwa amewahakikishia wawekezaji hao kuwa Serikali ya Tanzania iko tayari kwa uwekezaji wao na itawawezesha kuwekeza mitaji yao.

"Sisi tuna madini na ninyi ndugu zetu Wakorea mna mitaji. Twende tuunganishe nguvu kwa manufaa ya nchi zote," alisema Majaliwa alipokutana na ujumbe huo wa Korea Kusini juzi na kujadili kuhusu uhushirikiano katika uendelezaji wa madini ya kimkakati nchini.

"Ninapenda kuwahakikishia kuwa nchi yetu ni salama na Mheshimiwa Rais wetu Dk. Samia Suluhu Hassan anafanya kila linalowezekana kuboresha mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji nchini," alisema.

Waziri Mkuu alisema serikali imeimarisha mazingira ya uwekezaji ikiwa ni pamoja na kuboresha miundombinu ya usafirishaji kama barabara, ndege na nishati ya kutosha kwa ajili ya uendeshaji wa viwanda.

"Lengo ni kuhakikisha kila mwekezaji anayekuja anapata faida kutokana na uwekezaji wake," Waziri Mkuu alisema.

Mjumbe Maalum wa Rais wa Korea ambaye ndiye kiongozi wa ujumbe huo kutoka Korea Kusini, Yoon Sang Jick, aliishukuru Serikali ya Tanzania kwa kukabirishwa vizuri na wataendelea kushirikiana kuhakikisha malengo ya uwekezaji yanafanikiwa.

Waziri wa Madini, Anthony Mavunde, aliishukuru Korea Kusini kwa kuichagua Tanzania na kufanya mazungumzo kuhusu uwekezaji katika sekta ya madini.

Mavunde alitumia fursa hiyo kuwakaribisha wawekezaji kutoka Korea Kusini waje wawekeze Tanzania.



Mwasisi wa Taasisi ya Center to Advance Research on Health in Africa (CAReH Africa), Prof. Gbenga Ogedebde ambaye ni Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Grossman nchini Marekani, akitoa mada katika semina kuhusu kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia nchini iliyofanyika Zanzibar mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wanaharakati wamulika usawa kijinsia uongozi vyama vya siasa

**Na Beatrice Moses**

VUGUVUGU la wanaharakati wakiongozwa na Mtandao wa Jinsia (TGNP) wamesisitiza umuhimu wa kuzingatia usawa wa jinsia katika nafasi za uongozi wa vyama vya siasa.

Kwa miongo kadhaa nafasi za juu za uongozi ndani ya vyama vya siasa zimekuwa zinachukuliwa na wanaume, huku wanawake wakibaki kuwa wanachama au kupewa nafasi za chini za uongozi. Mwanaharakati Deogratusi Koyanga alilalamikia dosari hiyo ya kijinsia mwishoni mwa wiki alipozungumza na wahariri na waandishi wa habari wakati wa warsha iliyolenga kuzungumzia maandalizi ya Tamasha la 15 Kijinsia na Miaka 30 ya TGNP na Tapo la Kifeminia.

"TGNP kwa kushirikiana na wadau wengine tulihakikisha tunapaza sauti kwenye vyombo husika vya usimamizi ikiwamo Msajili wa Vyama vya Siasa kuhusu nafasi ya mwenyekiti na katibu ndani ya vyama vya siasa kumilikiwa na jinsi ya kiume.

"Tunashukuru tuliweka, sasa tunaona kuna mabadiliko kwa kuwa wanawake nao wanapewa au kuchaguliwa kwenye nafasi hizo," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP, Lilian Liundi, katika warsha hiyo, alisema mfumo dume ambao awali uligandamiza zaidi wanawake ndani ya jamii, sasa umebainika kuwaathiri hadi wanaume hasa wenye kipato cha kati na chini.

Liundi alisema mfumo huo umewajengea wanaume fikra za kupambana binafsi kutafuta kipato na kutunza familia, hata akikwama anaogopa kumshirikisha majukumu mkewe hata kama kamzidi kipato.

"Ni mfumo dume umewajengea hofu baadhi ya wanaume kujiunga na vikundi vya kuweka na kukopa kulinganisha na ushiriki wa wanawake ulivyo. Wanaume wanapambana kivyao tu, huku wakiwa wametawaliwa na hofu na kupoteza heshima ya uongozi ndani ya familia kwa kuwa wana kipato kidogo," alisema Liundi.

Kutokana na kampeni iliyofanywa ya kukomboa wanawake, wengi sasa wana elimu. Kwa hiyo, wapo walioajiriwa na wanalipwa vizuri, lakini kwa sababu ya mfumo dume, huwa hawawajibiki ipasavyo kugharamia majukumu ndani ya familia, hivyo inabaki kuwa wajibu wa mwanamume zaidi.

Ofisa Habari wa TGNP, Monica John, alisema jukwaa kubwa la ujenzi wa nguvu za wanaharakati linatarajiwa kushirikisha zaidi ya watu 15,000, mijadala mbalimbali itafanyika ikihusisha viongozi mbalimbali na wataalamu wa fani tofauti zinazohusu masuala ya ustawi wa jamii kwa kuzingatia usawa wa jinsia.

## Maofisa biashara, mazingira wanolewa athari za kemikali

**Na Mary Geofrey**

MAMLAKA ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) Kanda ya Mashariki imetoa mafunzo ya uelewa wa kemikali kwa maofisa biashara, maofisa mazingira na wadau wa kemikali katika Halmashauri ya Wilaya ya Kigamboni ili kuwajengea uelewa wa matumizi yake na kushirikiana katika utambuzi.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kigamboni, Ofisa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu, Tabia Nzowa, alisema juzi kuwa mafunzo hayo yamekuja wakati mwafaka kuwasaidia kutoa elimu ya matumizi salama ya kemikali kwa wadau katika halmashauri hiyo.

"Mafunzo hayo yametujenga katika uelewa wa matumizi ya kemikali na aina zake na hata kuweza kuitambua GCLA inayosimamia masuala ya kemikali.

"Niseme tu pia kwa halmashauri yatasaidia katika kuwaelimisha wananchi namna ya kuweza kuchukua tahadhari pindi wanapotumia kemikali," alisema Tabia.

Alisema elimu waliyopatiwa na itasaidia kuwatambua wafanyabiashara wanaojihusisha na matumizi ya kemikali husussani kipindi cha kukata na kuhuisha leseni zao za biashara, pia itakuwa rahisi kwa wao kuwashauri kujisajili Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali na kupatiwa kibali.

Meneja wa GCLA Kanda ya Mashariki, Danstan Mkapa, alisema mafunzo yaliyotolewa kwa maofisa hao wa Kigamboni yalilenga kuwapa uelewa wa kemikali na matumizi yake na kuweza kushirikiana katika usajili wa wadau wanaotumia kemikali ili kuhakikisha wanazingatia Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali Na. 3 ya Mwaka 2003.

Mkuu wa Divisheni ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji wa Halmshauri ya Wilaya ya Kigamboni, Hassan Pongwa, aliishukuru GCLA Kanda ya Mashariki kwa kutambua umuhimu wa kuwapatia mafunzo hayo kwa kuwa yamewaongezea kujua kemikali kwa mapana yake na kujua wadau wanaojihusisha na shughuli za kemikali katika halmashauri hiyo.

Katika mafunzo hayo, mada mbalimbali ziliwasilishwa kwa maofisa hao, ikiwamo ya kutambua aina mbalimbali za kemikali wanazosafarisha pamoja na athari za kiafya na mazingira zinazoweza kuletwa na kemikali.

## Wanafunzi wapewa kompyuta kuwezesha somo la TEHAMA

**Na Mary Geofrey**

WANAFUNZI wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Zanaki sasa wana uhakika wa kujifunza somo la Teknolojia ya Habari na Mawasilino (TEHAMA) kwa vitendo baada ya kupokea msaada wa kompyuta 30.

Msaada huo wa kompyuta na vifaa vyake ulitolewa na Kampuni ya Trade Dest kwa kushirikiana na Taasisi ya TEHAMA kwa Wote mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam.

Mkuu wa shule hiyo, Delvine Koka, akizungumza baada ya kupokea msaada huo, alisema zitawasaidia wanafunzi kusoma kwa vitendo somo la TEHAMA.

"Kompyuta hizi zitasaidia kufanikisha somo la ICT kueleweka kwa urahisi na ufanisi mkubwa shuleni hapa. Msaada wa mashine ya madurufu nao utatusaidia kwenye kazi za ofisi," alisema Koka.

Mwakilishi wa Ofisa Elimu Mkoa wa Dar es Salaam, Pilly Ngalambe, alisema msaada huo utawezesha wanafunzi hao kujifunza kwa vitendo somo hilo ili kuendana na kasi ya dunia.

"Wadau hawa kutushika mkono ni jambo jema la kuunga mkono juhudi za serikali katika kuwezesha watoto wa kike kupata elimu hasa ya TEHAMA," alisema.

Katibu wa Taasisi ya TEHAMA Kwa Wote, Avelin Malamshi, alisema msaada huo ni mwendelezo wa jitihada zao katika kurudisha fadhila kwa jamii. "Hii ni shule yetu ya nne kutoa msaada huu, kwa sababu tunaamini katika kurudisha fadhila kwa jamii kutoka kwenye faida tunayopata," alisema.

Alibainisha kuwa wameshatoa elimu ya kompyuta kwa walimu 200 wa shule mbalimbali nchini ili kusaidia kufundisha masomo hayo kwa wanafunzi wao.

Mwanafunzi wa shule hiyo, Anna Komba, alisema wamepokea msaada huo wakiamini utawasaidia kwa kiasi kikubwa kujifunza masomo yanayohitaji kompyuta.



## HABARI KANDA KASKAZINI

# Umaskini Longido washuka kutoka asilimia 77 hadi 37

**Na Daniel Sabuni,** LONGIDO

HALI ya umaskini ngazi ya kaya kwenye vijiji 19 vya Tarafa ya Ketumbeine, Wilaya ya Longido mkoani Arusha, imepungua kutoka asilimia 77.6 hadi kufikia 37.1.

Jitihada hizo zimetokana na Shirika la Kimataifa la World Vision kuweka nguvu zake kwa miaka 14 kupambana na umasikini huo.

World Vision Tanzania, ilianzisha juhudi za makusudi za kukabiliana na umasikini huo mwaka 2009, kupitia Mradi wa Ketumbeine AP.

Mkurugenzi Mkuu wa World Vision Tanzania, James Andit, wakati anakabidhi rasmi mradi huo kwa serikali mwishoni mwa wiki, alisema kazi ya kupunguza umasikini katika jamii ya Ketumbeine, halikuwa jambo rahisi, kwa kuwa jamii ilihitaji elimu na uhamasishaji zaidi ili kuwatoa walipo na kuwapeleka kwenye dhumuni halisi la mradi. Andit alisema shirika hilo halitafunga mradi isipokuwa limeukabidhi kwa wananchi na serikali ili kuundeleza pale walipofikia ili kuendelea kupunguza umaskini kwa wananchi, kwa kumlenga mtoto anayeishi katika mazingira magumu.

Kabla ya makabidhiano hayo, Mwenyekiti wa Kijiji cha Orkeju-Loongishu na Mjumbe wa Bodi ya Mradi wa Ketumbeine AP, Lekishon Kaika, alimweleza Mkuu wa Wilaya ya Longido, Marco Ng'umbi, kuwa kipimo cha kupungua kwa umaskini, kimejulikana kutokana na utafiti uliofanywa kabla ya mradi na Shirika la World Vision. World Vision imetekeleza miradi ya mafanikio ya kilimo, mifugo na vikundi vya kukopeshana ambavyo vimeacha alama kwa kuongeza tija kwa kuinua uchumi kwa wananchi 51,877 wa kata sita za Ketumbeine, Noondoto, Elagh'tadapash, Ilerienito, Gilaimerugoi na Gilailumbwa.

"Uuzaji wa mifugo, mazao na vikundi va VICOBA na upatikanaji wa mikopo yenye masharti nafuu vimechochea sana biashara za kuuza mifugo na mazao ya kilimo.

... Pia umechochea shughuli zisizo za kilimo au mifugo kama migahawa /mamalishe na usfirishaji abiria kwa kutumia pikipiki maarufu bodaboda" alisema Kaika.

Alisema mradi wa kilimo, mifugo na uchumi lengo lake ni kuchangia upatikanaji wa chakula na kipato kupitia ongezeko la uzalishaji katika kilimo, mifugo na biashara.

Aidha, unalenga kuchangia ustawi wa watoto na kuwawezesha wazazi kuwa na uwezo wa kuhudumia watoto wao na wanafamilia wengine kupitia uchumi imara, ufugaji na kilimo bora.

Katika juhudi za kupunguza umaskini katika eneo la Ketumbeine, ambalo miaka mitatu mfululizo limekumbwa na ukame, huku wakazi wake wakitegemea asilimia 81 ya mifugo kama shughuli kuu ya uchumi, Shirika la World Vision, limewawezesha mifugo 6,105, ikiwamo mbuzi, ng'ombe na kondoo wanaovumilia ukame.

Kaya zilizonufaika ni 3,834 ambapo watoto walikuwa wanaishi katika mazingira duni.

"Tarafa yetu kuna ongezeko ya asilimia ya wazazi wanaomudu mahitaji ya watoto wao kutoka asilimia 43 (2009) mpaka asilimia 72.5 kwa sasa," alisema mjumbe huyo.

Alisema pia mradi uliwezesha kuundwa kwa vikundi vya wakuweka na kukopa (VICOBA) 175, vyenye wanachama 4,018, wanawake wakiwa 2,988 na wanaume 1,030 ambavyo vimeweka akiba ya thamani ya zaidi ya Sh.bilioni 1.6.

Kuhusu mradi wa afya na lishe alisema shirika limewakomboa baada ya kuwajengea uwezo wa kila namna, kuhamasisha na kufanikiwa kujenga Kituo cha Afya cha Ketumbeine, kwa kushirikiana na wananchi jambo linalosaidia mama na mtoto kupata huduma bora na kupunguza vifo vya wajawazito vilivyotokana umbali kutoka vijiji hadi hospitali.

"Hivi sasa tuna zahanati 12 katika tarafa yetu, mwanzo wananchi walikuwa wakifuata huduma kwa kutembea umbali wa takribani kilomita 10 mpaka 15 hali iliyokuwa ikisababisha vifo kutokana na kuchelewa kupata huduma" alisema.

Alitaja miradi mingine kuwa ni maji na usafi wa mazingira, elimu, ufadhili, ulinzi wa mtoto na utetezi.

Alisema mradi umefanikisha kujenga madarasa na vyumba za walimu katika vijiji vya Tarafa ya Ketumbeine, mabwawa ya kunyweshea mifugo na kupunguza kwa kiasi kikubwa ndoa za ututoni kwa wananchi wa jamii ya kimasai.

"Mwaka 2009 tulipokuwa tukianza mradi watoto wakike waliozwa katika umri mdogo sana, mtoto wa miaka 8 anaozwa kwa mzee wa miaka 70, tumepeleka elimu kwa wananchi na sasa tatizo hili limepungua kwa kiasi kikubwa sana, kuthibitisha hili idadi ya watoto wa kike wanaoandikishwa shule ya msingi imeongezeka pamoja na mahudhurio kwa wafunzi wote katika tarafa hii kufikia 98% kutoka 58," alisema Peruth Daud, mratibu wa mradi.

Baada ya makabidhiano hayo, Mkuu wa Wilaya hiyo, Marco Ng'umbi, alilishukuru shirika hilo kwa mradi mkubwa uligharimu zaidi ya Sh.bilioni 15.




Baadhi ya wadau wakiwa na watu wenye tatizo la uti wa mgongo wakimsikiliza mgeni rasmi Ofisa Ustawi wa Jamii wa Mkoa wa Kilimanjaro, Scolastica Swai (hayuko pichani), katika ufunguzi wa elimu kwa jamii kuhusu matatizo ya uti wa mgongo iliyoandaliwa na Shirika la Songambele Initiative mwishoni mwa wiki. **PICHA: JAMES LANKA**

# Wakazi wengine Ngorongoro waomba kuondoka

**Na Allan Isack,** NGORONGORO

BAADHI ya wakazi wa vijiji vya lrkeepusi na Orchaniomelok vilivyoko ndani ya eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), wameridhia kuhama katika makazi yao ya asili na kuhamia Msomera, Wilaya ya Handeni, mkoani Tanga kwa hiari.

Wamesema wameridhia kuhama baada ya kupata fursa ya kuwatembelea wenzao waliohama eneo hilo.

Samweli Lazier, Mkazi wa lrkeepusi, Kata ya Nainokanoka, alisema amepata fursa ya kuwatembele wenzake na ameridhishwa na mazingira wanayoishi.

"Nilipofika Msomera, nimekuta wenzetu waliotoka huku Ngorongoro wanafanya shughuli zao mbalimbali za kujipatia kipato ikiwamo kilimo, ufugaji na biashara ndogo ndogo kwa kuwa ni sehemu ambayo mtu anakuwa na uhuru kufanya shughuli yoyote, pia kuna huduma muhimu za kijamii," alisema.

Naye Gesuma Turmeyi, alisema kutokana na uzuri wa eneo ambalo wanalitakiwa kwenda kuishi, ameiomba serikali kuharakisha utaratibu wa walioiandikisha ili waondoke.

Metuo Setayi, Mkazi wa Kijiji cha Orchaniomelok, Kata ya Alalilai, alisema anataka kuondoka ndani ya eneo la NCAA, kwa kuwa amekumbana na changamoto mbalimbali ikiwamo kupoteza mifugo yake iliyouawa na wanyama wakali wa porini.

# RC amaliza mgogoro wa ardhi uliodumu miaka mingi

**Na Hamida Kamchalla,** KILINDI

MKUU wa Mkoa wa Tanga, Waziri Kindamba, amefanikiwa kuruka mtego wa Rais Samia Suluhu Hassan, baada ya kutatua mgogoro uliodumu kwa miaka mingi uliohusu mipaka ya kiutawala kati ya vijiji vya Gitu na Ngobole vilivyoko Wilaya ya Kilindi.

Akiwa katika Kijiji cha Gitu, Kindamba alimaliza mgogoro huo na kusema kuanzia siku hiyo, hataki kusikia mgogoro wowote ukiendelea na atakayejaribu hatavumiliwa kwani eneo linalogombaniwa litakuwa chini ya Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ).

Alisema mgogoro huo unahusisha vitongoji viwili vya Komtindi na Ngaloji ambao umedumu kwa miaka 17 ukiwa na utata wa kila kijiji kudai vitongoji hivyo viko upande wake, lakini uhalisia vinapata huduma zote za kijamii kutoka Kijiji cha Gitu na pia ramani inaonesha hivyo.

Aidha, Kindamba aliwaasa wananchi kwamba suala la kupambana na kusuhisha migogoro siyo kipaumbele chake bali ni kuhakikisha anawaletea maendeleo hususani barabara ambazo zitaunganisha mawasiliano na kufungua uchumi wa Mkoa wa Tanga na kwa faida ya taifa.

Alisema: "Tusiumizane kichwa mimi nina mambo mengi ya kufanya hasa katika kuwaletea wananchi wa Tanga maendeleo, sisi tunatakiwa kuangalia mbele kila mmoja kwa nafasi yake na kupambana kujua hii Barabara ya Handeni - Kilindi - Kiberashi hadi Kiteto,

"Tuombe hivyo kwasababu hii barabara itakapokamilika watakaokuwa wanataka kwenda Bandari ya Dar es salaam wasiende huko, waje Bandari Tanga, barabara iwe inafanya kazi muda wote, watu walime na biashara ziende kwenye masoko," alisema. "Sisi tuna ardhi yenye rutuba, lakini kwasababu akili yetu tunaishuhulisha kwenye migogoro, acheni na baada ya kikao cha leo tutashuhulika nae sisi kama serikali, hatutaki kusikia mgogoro huu tena," alisisitiza.

Alisema: "Kati ya Gitu na Ngobole, katikati kuna msitu upo pale, eneo lile tunawakabidhi Jeshi la Wananchi (JWTZ) na tangu awali walishaliomba lakini serikali haikuwapatia, kwahiyo mkiwaona wanazunguka pale, wapo kwenye maeneo yao wanafanya mazoezi," alisema.

Kindamba, aliagiza serikali za vijiji hivyo kukaa na kutengeneza muhtasari kuhusu maamuzi aliyotoa kwenye kikao hicho ambapo alimsisitiza Mkuu wa Wilaya hiyo, Hashimu Mgandilwa kuwasimamia wenyeviti hao.

Hata hivyo, aliwataka wenyeviti wa vijiji kuacha tabia ya kuuza ardhi bila kufuata taratibu kwani mihuri wanayotumia ilishapigwa marufuku, hivyo atakayefanya hivyo hatua kali zitachukuliwa dhidi yake bila kuonewa huruma.







Waendesha pikipiki mkoani Tabora wakipanga foleni kwenye kituo cha mafuta ya petroli na dizeli wakisubiri kupatiwa huduma kutokana na baadhi ya vituo kukosa mafuta kwa kile kinachoelezwa kusababishwa na uhaba wa dola nchini. **PICHA: HALIMA IKUNJI**

# Wamabondeni waanza kujihadhari mvua ya El-Nino

**Na Neema Charles,** SAUT

BAADHI ya wananchi na wakazi wa maeneo ya jirani na Ziwa Victoria na wanaoishi maeneo ya mabondeni mkoani Mwanza wamejipanga kukabiliana na mvua ya El-Nino inayotarajiwa kuanza mwezi huu.

Hatua hiyo inatokana na tahadhari iliyotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Nchini (TMA) kwa kutangaza kutarajiwa mvua ya El-Nino inayokadiriwa kuisha Aprili mwakani na maeneo yatakayoathirika ni ya mabondeni na kando ya vyanzo vya maji.

Wakizungumza na Nipashe iliyotembelea maeneo hayo kwa nyakati tofauti, wananchi hao walisema tahadhari walizozipa kipaumbele zaidi ni zile za dharura katika kuhakikisha wanaweza kujiokoa katika maeneo yao kwa kuwa uwezo wa kuhama maeneo husika.

Rahabu Shigella, mkazi wa eneo la bondeni, Kata ya Mabatini, alisema wameanza kuboresha miundombinu ya choo ambayo ina shida kipindi cha mvua na kusababisha magonjwa ya milipuko.

"Pamoja na mambo mengine tumeamua kuweka miundombinu ya vyoo vyetu kuwa kwenye hali salama pia kwa majirani zetu waliopo katika maeneo ya milima maana wakati wa mvua hutapisha vyoo vyao na kuleta athari kwetu tulio mabondeni," alisema.

Mkazi wa Capripoint, Bismark Sirkodie alisema amejihakikishia mawasiliano ya karibu na watoa huduma za dharura kwa usalama wa familia yake ikiwa ni pamoja na mawasiliano na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na wahuduma wa afya.

Mkazi wa Nyegezi, Dativa Dastani, alisema kutoka na dharura hiyo wananchi na wakazi wa maeneo ya bondeni walitakiwa kuhama kuepuka madhara.

Mmoja wa wakazi wa eneo la bondeni ambaye hakutaka jina lake litajwe gazetini, alisema kwao kuhama katika kipindi cha mvua ni kawaida na kwa sasa wamejipanga kuhama na kwenda kupanga kwa muda katika maeneo ya juu ili kuokoa uhai wao na mali zao.

"Shida tunayokabiliana nayo ni kwa watoto wetu wanaoendelea na masomo baada ya kuhama wanatembea umbali mrefu kuzifuata shule, lakini kwa sasa tunajitahidi kusikiliza kwa karibu taarifa hizi za hali ya hewa ili pale tutakapohitajika kuhama tufanye hivyo," alisema.

Taarifa iliyotolewa na TMA mwezi Agosti, ilisema miongoni mwa madhara yatakayojitokeza kutokana na mvua hiyo ni pamoja na matukio ya vifo, magonjwa ya mlipuko na uharibifu wa miundombinu hususani katika kipindi cha Oktoba hadi Desemba 2023.

# IFAD yataka uboreshaji miundombinu umwagiliaji

**Na Neema Emmanuel,** MAGU

MAKAMU wa Rais wa Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD), Donal Brown, ameahidi kurejea nchini Tanzania kwa ajili ya kukagua utekelezaji na kuboresha miundombinu ya umwagiliaji katika miradi ya kilimo na ufugaji wilayani Magu hali itakayowasaidia watekelezaji wa miradi hiyo kufikia malengo kwa wakati. Alitoa kauli hiyo juzi wakati wa ziara yake wilayani humo ya kukagua miradi ya ufugaji wa kondoo, kilimo cha mihogo na visima kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji, kunyweshea mifugo na matumizi mengine ya kibinadamu.

Alisema tatizo kubwa aliloligundua ni ukosefu wa maji na anatarajia kurejea nchini kuangalia utekelezaji wa visima vya maji ili kujiridhisha na mafanikio katika miradi hiyo.

"Miradi hii ni sehemu ya ufumbuzi wa matatizo yanayowakabili wananchi na ni muhimu na yenye fursa tunatarajia kuwa na mkutano mkubwa wa kimataifa Afrika wa kuangalia usalama wa chakula na uzalishaji wake kitafanyika hapa nchini lengo ni kuhakikisha wananchi wananufaika ipasavyo na kilimo na ufugaji," alieleza Brown.

Katibu wa kikundi cha maendeleo ya jamii Lumeji chenye mradi wa ufugaji kondoo, Evarist Pamba, alisema kutokana na ardhi kuharibika na ukosefu wa maji imesababisha upatikanaji mdogo wa mazao na kujikita katika shamba darasa la ufugaji wa kondoo ili kuvuna mbolea zaidi na kurejesha rutuba ya udongo. Joseph Kihaule Mratibu wa mradi wa kitaifa, alisema miradi hiyo ipo kimkakati katika kuongeza usalama wa chakula na kutunza mazingira huku wilaya hiyo ikipokea zaidi ya Shilingi bilioni moja kutekeleza miradi na kuwanufaisha watu 3,000 moja kwa moja na 7,000 wasio wa moja kwa moja. Emil Kasagara, Kaimu Katibu Tawala Mkoa, alisema serikali imeweka mazingira rafiki ambayo yanachangia wahisani kuja kufadhili maendeleo ya wananchi na kuwaletea faida na kuimarisha usalama wa chakula.

## Gharama kubwa upimaji shirikishi viwanja yalalamikiwa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

GHARAMA ya awali ya upimaji wa eneo katika maandalizi ya upatikanaji shirikishi na hatimiliki, imekuwa kikwazo kwa baadhi ya wakazi wilayani Kahama na kuamua kujenga makazi ya kudumu kiholela kwa kutofuata utaratibu hali inayoibua migogoro ya ardhi ya mara kwa mara.

Diwani wa Nyahanga Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, Pancrasi Ikongolo, aliyabainisha hayo jana wakati wa kikao cha wadau kujadili utekelezaji wa Mradi wa Uboreshaji wa Miliki za Ardhi (LTIP) unaotekelezwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa ufadhili wa Benki ya Dunia kwa zaidi ya Sh. bilioni 300.

Alisema, moja ya sababu wananchi wengi kujenga makazi yao ya kudumu kiholela, ni gharama ya Sh. 90,000 ya upimaji wa maeneo yao kabla ya ujenzi

"Kata hii ina mitaa minne kati ya hiyo mtaa wa Mtakuja unaongoza kwa migogoro ya ardhi hasa ya kuuza kiwanja kimoja kwa watu wawili, uvamizi wa maeneo ya wazi na taasisi za umma," alisema Ikongoli.

Mkazi wa Mhungula, Scholasitika Bebete, alisema wajane wengi walipokonywa mali na maeneo yao kwasababu ya kutokuwa na hatimiliki baada ya wenza wao kuondoka.

Mkuu wa Idara ya Ardhi Manispaa ya Kahama Clemensi Mkusa alisema, wamejipanga kutekeleza mradi huo ipasavyo na jumla ya mitaa 17 itafikiwa na kurathimishwa maeneo na kutoa hatimiliki zaidi ya 43,000 bila gharama hiyo ya Sh. 90,000 na kuwataka madiwani kuwahamasisha wananchi kutoa taarifa za uhakika za maeneo yao kwa sababu mradi hautakuwa nafidia yoyote.

Meneja wa Urasimishaji Mjini wa mradi huo, Leons Mwenda, alisema Bunge la mwezi Juni mwaka huu lilishusha viwango vya gharama za utengenezaji wa hati miliki ikiwamo maombi ya hati, ada na ada ya ramani ndogo ya hati ya Sh. 20,000 na kuwa Sh. 5000 ambayo inalalamikiwa na wananchi.

Hata hivyo, alisema ada ya hati ilikuwa Sh. 50,000 na sasa ni Sh. 25,000 na katika utekelezaji wa mradi huo wananchi watatakiwa kulipa malipo ya asilimia 0.25 kulingana na ukubwa wa eneo husika.

Mkurugenzi wa Mipango Miji kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Degratius Kalimenze, alisema, mradi umelenga kuboresha usalama wa miliki za ardhi kwa kupanga, kupima na kusajili miliki za ardhi zipatazo milioni 2.5 zitakazojumuisha hatimiliki milioni moja, leseni za makazi milioni moja katika maeneo ya mijini na hati za kimila 500,000 vijijini.

Nipashe
Spotika



WACHEZAJI WA5 GHALI WANAOTAKIWA KUTHIBITISHA THAMANI YAO DIMBANI UK. 12-13




# MATATIZO MA3 MAKUBWA YANAYOISUMBUA CHELSEA

**LONDON,** England

CHELSEA ilichapwa mabao 3-1 na West Ham United Jumapili ya Agosti 20. Kilikuwa kipigo chao cha kwanza msimu huu, baada ya sare ya 1-1 dhidi ya Liverpool Uwanja wa Stamford Bridge wikendi ya ufunguzi.

West Ham walichukua uongozi kabla ya Carney Chukwuemeka wa Chelsea kuwasawazishia 'The Blues' hao katika kipindi cha kwanza. Chelsea ilishuhudia Enzo Fernandez akikosa mkwaju wa penalti kuelekea mapumziko.

The Blues walishambulia zaidi katika kipindi cha pili, lakini waliondolewa katika shambulizi la kushtukiza, huku Michail Antonio akiifungia West Ham.

Mechi hiyo ilichukua mkondo mwingine huku West Ham ikipunguzwa hadi wachezaji 10 muda mfupi baadaye, lakini Chelsea ikashindwa kutumia fursa hiyo. Badala yake, walikuwa ni 'Wagonga Nyundo' hao waliofunga bao la tatu, huku Lucas Paqueta akifunga.

Hadi mwisho wa mchezo, Chelsea walionekana kurudi kwenye njia zao za zamani za msimu uliopita bila mpangilio na kuchanganyikiwa.

Ingawa ndio kwanza msimu umeanza, mashabiki wa Chelsea wanajua kwamba nini kinaweza kutokea, hasa kutokana na matokeo ya msimu uliopita.

Dalili za kushindwa kubadilisha nafasi za kufunga tu kwenye mashambulizi ya kaunta ndizo zilizoikumba Chelsea msimu uliopita na inaonekana kuendelea na mwenendo huo safari hii pia.

Kwa maelezo hayo, hebu tuangalie matatizo matatu makubwa ya Chelsea kwa sasa...

**#1 Shughuli nyingi za uhamisho**

Chelsea wameongoza uhamisho mkubwa kwa klabu msimu huu wa majira ya joto na wakati huo huo kuleta wachezaji kadhaa wapya. Wametumia gharama kubwa kwenye dirisha la tatu mfululizo na kikosi kinaonekana kufanyiwa marekebisho makubwa kabisa.

Kwenye daftari la mishahara, inaonekana ni hatua nzuri, kwani sasa wana wachezaji wenye umri mdogo wanaolipwa mishahara midogo na bonasi zinazotokana na utendaji kazi, lakini matumizi ya jumla ya uhamisho sasa yanakaribia pauni bilioni moja.

Zaidi ya hayo, Chelsea sasa wana suala la kulazimika kuunganisha timu ambayo wote ni wapya katika klabu hiyo. Kikundi cha vijana huenda kitakua baada ya muda na kuwa wachezaji wa kutisha, lakini kwa wakati huu ni zaidi ya upande usiounganishwa na vijana, ambao hawana uzoefu wa kushinda michezo katika Ligi Kuu England.

Wachezaji kama Romeo Lavia, Moises Caicedo, Fernandez, Mykhailo Mudryk, Christopher Nkunku na wengine wamesajiliwa lakini wameletwa mwaka huu.

Hii inamaanisha kuwa hawajapata wakati unaohitajika wa kuunda kemia na kuzoea mtindo wa kucheza pamoja. Kwa kuongezea, wachezaji hawa wako kwenye mikataba mirefu kupita kiasi, ikimaanisha kwamba ikiwa hawatafanikiwa, itakuwa ngumu kuwaondoa.

**#2 Kuondoka kwa wachezaji**

Hiyo inatuleta kwenye hatua yetu inayofuata. Kurejea kwenye kikosi kilichoshinda Ligi ya Mabingwa Ulaya miaka miwili iliyopita na ni nyota kama Recce James, Thiago Silva na Ben Chilwell pekee waliosalia katika klabu hiyo. Suala hapa ni kwamba, kikosi cha kwanza hakitambuliki mwaka jana na uliopita.

Wachezaji wa kikosi cha kwanza kama vile Kai Havertz, Mason Mount, Mateo Kovacic, N'Golo Kante, Edouard Mendy na zaidi waliuzwa.

Zaidi ya hayo, mengi ya majina haya yaliuzwa kwa wapinzani kama vile Manchester City, United na Arsenal. Ingawa hilo si jambo baya, lakini urekebishaji wa vikosi viwili ndani ya misimu miwili hautoi picha ya utulivu. Inapunguza uzoefu kidogo kutoka kwa upande huku ikifanya iwe ngumu kwa kocha kupata kile anachokitaka.

**#3 Mauricio Pochettino anaweza kuwa hafiti**

Tukizungumzia makocha, Chelsea ilichukua hatua nyingine kubwa katika kumteua kocha huyo wa zamani wa Paris-Saint Germain. Mauricio Pochettino ni miongoni mwa majina ya makocha maarufu na kazi yake katika klabu za awali kama vile Southampton na Tottenham ilikuwa ya kupigiwa mfano. Hata hivyo, alipewa muda mwingi wa kupata mawazo na mbinu zake na kuunda upande wake.

The Blues hawana huruma linapokuja suala la kuachana na kocha na huwa hawapewi nafasi nyingi sana.

Thomas Tuchel alifukuzwa mapema msimu uliopita na mrithi wake Graham Potter hakuweza hata kuona kumaliza msimu huku Frank Lampard akichukua jukumu la muda.

Kwa hiyo, inaonekana kama Chelsea inaweza kuwa imemfuata kocha ambaye labda hajazoea kushughulikia mradi unaozingatia wakati.

Kwa bahati mbaya, ni wakati ambao kikosi hiki kinahitaji, bila kujali kocha ni nani.

**ISIKUPITE**

USAJILI wa ghali zaidi katika historia ya Klabu ya Real Madrid, Eden Hazard (Euro milioni 115), Jude Bellingham (Euro milioni 103), Gareth Bale (Euro milioni 101) na Cristiano Ronaldo (Euro milioni 94).



# WACHEZAJI WA5 GHALI WANAOTAKIWA KUTHIBITISHA THAMANI YAO DIMBANI



RASMUS HØJLUND

**LONDON,** England

DIRISHA la usajili wa wachezaji kipindi cha majira ya joto Ulaya limekamilika mwishoni mwa wiki.

Klabu zote barani Ulaya zimefanya harakati ya kusajili wachezaji kwa fedha nyingi na kuuza wale wasiohitajika ili kufikia malengo yao ya msimu huu.

**Kadiri fedha zinavyotumika, kuna masimulizi kadhaa ya kawaida na yasiyo ya kawaida kuhusu dirisha hili la uhamisho.**

Sawa na misimu iliyopita, Klabu za Ligi Kuu England hazijaepuka tabia zao za matumizi makubwa ya fedha, kwani klabu kama Arsenal, Chelsea, Manchester United na Manchester City zimeweka nguvu zao za kifedha ili kuvutia baadhi ya majina ya juu kwenye mchezo huo.

Majina kama Declan Rice, Moises Caicedo, Josko Gvardiol na Rasmus Hojlund yamesajiliwa. Newcastle United ndio timu iliyoingia kwenye orodha ya hivi karibuni ya kutumia fedha nyingi ikiwa imemsajili Sandro Tonali.

Real Madrid pia wamefanya usajili wa Jude Bellingham wakati Barcelona nao hawako nyuma.

Uhamisho wa Bayern Munich kwa Harry Kane pia ulikuwa gumzo msimu huu wa majira ya joto alipoondoka Tottenham Hotspur. Kipengele kingine cha kuvutia kimekuwa shughuli kutoka kwa klabu za Saudi Arabia ambazo zimevutia baadhi ya wachezaji wakubwa wa Ulaya kwa ada kubwa na mishahara minono.

Tumeona uhamisho wa wachezaji wanne ukivunja rekodi ya euro milioni 100. Hata hivyo, wengi wa wachezaji hawa watalazimika kuonesha thamani yao ili kuhalalisha ada zao za uhamisho ambazo klabu zao zimetozwa...

## #1 Declan Rice - West Ham kwenda Arsenal

Mhitimu wa akademi ya Chelsea, Declan Rice, alikuwa na wakati mzuri zaidi kule West Ham United. Katika misimu michache iliyopita, kiungo huyo wa kati wa England alibadilika na kuwa mchezaji anayetoa zaidi katikati ya Uwanja wa 'Wagonga Nyundo' hao wa London na hivyo alizawadiwa nafasi ya kuichezea Timu ya Taifa ya England katika michuano miwili iliyopita ya kimataifa.

Rice alikuwa mchezaji anayesakwa miongoni mwa klabu za juu kama Chelsea na Manchester United wakionesha nia. Badala yake, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, akapewa jukumu la kukiongoza kikosi cha Mikel Arteta, Arsenal huku wakitumaini kwenda hatua moja zaidi katika Ligi ya England na kurejea Ligi ya Mabingwa Ulaya. Kwa ada kubwa ya euro milioni 116.60 iliyotumika katika uhamisho huo, kutakuwa na mengi kwenye mabega ya Rice.

## #2 Jude Bellingham - Borussia Dortmund kwenda Real Madrid

Tangu siku zake za awali kule Birmingham, Jude Bellingham amekuwa akipendekezwa kuwa mchezaji bora wa baadaye. Nia ilikuwa kubwa kwa chipukizi huyo kwani klabu kama Manchester United ilitafuta saini yake. Lakini alichagua kuondoka England na alihisi kuwa Dortmund pangekuwa mahali pazuri pa kujiendeleza zaidi.

Kwa kuzingatia rekodi ya klabu hiyo ya Ujerumani ya kuendeleza vijana, halikuwa jambo la kushangaza sana. Kwa muda mfupi aliokaa huko, alikuwa kiungo wa kiwango cha juu ambaye alikuwa akihitajika kila sehemu.

Liverpool walipigania sana usajili wake, lakini mvuto wa Real Madrid uliweza kushawishi akili yake kwa ada ya uhamisho ya euro milioni 103. Bellingham atakuwa na jukumu la kufufua safu ya kiungo ya Real kwa siku zijazo na tayari katika mechi nne tu za La Liga amecheka na nyavu mara tano, mwanzo mzuri kwa kinda huyo.

## #3 Moises Caicedo - Brighton kwenda Chelsea

Kinda huyo wa ajabu wa Ecuador hafahamiki kwa wale walio kwenye Ligi Kuu ya England. Hata wakati Brighton ilipomsajili misimu miwili iliyopita kutoka Independiente, walitoa kiasi kikubwa kwa mchezaji ambaye bado yuko katika ujana wake. Bila kujali, maendeleo yake chini ya Roberto de Zerbi yalimaanisha kwamba alihusika katika mzozo mkali wa uhamisho kati ya wapinzani Chelsea na Liverpool.

Brighton ilishikilia uthamini wao na nia yao ilikuwa wazi - kuuza kwa bei ya juu zaidi. Todd Boehly na Chelsea hatimaye walishinda mbio hizo, lakini ukiwa ni uhamisho wa pili ghali zaidi wa euro milioni 116 na bila shaka utakuwa na uzito mkubwa kwa kijana mwenye umri wa miaka 21 ambaye ana msimu mmoja tu kwenye Ligi Kuu England.

## #4 Rasmus Hojlund - Atalanta kwenda Manchester United

Manchester United walikuwa wakihitaji sana mshambuliaji mpya na chipukizi baada ya uchezaji wa Cristiano Ronaldo na Wout Weghorst msimu uliopita. 'Mashetani Wekundu' walijaribu kuwafuata Harry Kane na Victor Osimhen, lakini waliishia kwa raia huyo wa Denmark ambaye alikuwa na msimu mzuri kule Serie A.

Hojlund atakuwa akikabiliwa na maswali mengi kuhusu uhamisho huo sio tu kwa euro milioni 75 iliyolipwa na United. Bado ana umri wa miaka 20, lakini mabao 10 katika mashindano yote msimu wake wa kwanza kwenye ligi ya daraja la juu yanaweza kupendekeza kwamba United inaweza kuwa na malipo makubwa zaidi. Kuongeza kwa hilo changamoto za kuhama kutoka Serie A hadi Ligi Kuu England, inaweza kumfanya kuwa na wakati mgumu mbeleni.

## #5 Romeo Lavia - Southampton kwenda Chelsea

Kama vile Caicedo, Romeo Lavia alikuwa nyota wa msimu uliopita. Licha ya Southampton kushuka daraja, kijana huyo wa Ubelgiji alifanikiwa kujijengea jina la kuwa kiungo mkabaji na mwenye akili. Jambo lingine linalofanana na la Caicedo ni kwamba Chelsea na Liverpool zilipambana kuwania huduma yake.

Ilionekana kuwa karibu kutua kwa 'Wekundu wa Anfield', lakini Chelsea walifanikiwa kumchukua Lavia. Ni kweli Lavia ni kiungo mwenye kipaji, lakini bei ya euro milioni 62.1 kwa mchezaji asiye na uzoefu ni kamari ya uhamisho. Atakuwa makini wakati Chelsea inaanza ujenzi upya chini ya msimu wa pili wa mmiliki, Todd Boehly.

## Nukuu

"Naamini Cristiano Ronaldo ndiye alianzisha haya yote na kila mtu alimuita 'kichaa' na hili na lile, leo unaona ligi inazidi kukua zaidi na zaidi, itakuwa na ushindani mkubwa hasa baada ya usajili uliofanyika kwenye dirisha la usajili la majira ya kiangazi," **Neymar akieleza kushangazwa na ushindani uliopo Ligi Kuu Saudi Arabia baada ya kujiunga na Al Hilal, huku akikiri Ronaldo ndiye chanzo cha mastaa wengi kutua huko.**




"Messi anapaa na Inter Miami baada ya mechi sita pekee na hilo halinishangazi kutokana na ubora alionao, na kwa kuwa anacheza ligi dhaifu kuliko Ulaya," **Nyota wa zamani wa Barcelona na Brazil, Rivaldo.**



"Sema Salam Aleykum na watakuongezea Euro 500! Katika mshahara wako," **Ujumbe wa nyota wa PSG, Achraf Hakimi, akimtania Neymar wakati wakiagana alipokuwa akielekea kujiunga na Al-Hilal ya Saudia.**






Kiungo mshambuliaji wa Yanga, Pacome Zouzoua, akiwatoka mabeki wa KMC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam Agosti 23, mwaka huu na Yanga kushinda mabao 5-0. **MPIGAPICHA WETU**

# YANGA, AZAM ZATISHA REKODI LIGI KUU BARA

**Na Adam Fungamwango**

MECHI za raundi ya pili za Ligi Kuu Tanzania Bara zimekamilika huku jumla ya mabao 38 yakifungwa mpaka sasa, Yanga ikiongoza kufunga kipindi cha pili na Azam cha kwanza.

Jumla ya mabao 21 yamefunga kipindi cha pili, huku cha kwanza yakipachikwa 17 mpaka sasa ambapo ligi imesimama kwenye raundi hiyo kupisha mechi za kimataifa zilizo kwenye Kalenda ya FIFA.

**Takwimu zinaonesha kuwa kwa idadi ya mechi 16 zilizochezwa mpaka sasa, 11 zimetoa mshindi na sare tano mpaka sasa. Kati ya hizo, mechi nane timu zimeshinda nyumbani na tatu zimeshinda ugenini.**

Hata hivyo, kwa mujibu wa dawati la takwimu la Nipashe, mabao 38 yaliyofungwa kwenye Ligi Kuu msimu huu mpaka kufikia raundi ya pili yameshindwa kufikia rekodi ya msimu uliopita ambapo jumla ya mabao 40 yalipatikana mpaka kufikia raundi hiyo.

Katika makala haya tumekusanya takwimu mbalimbali za ligi hiyo hadi kufikia raundi ya pili, twende sasa...

**Yanga wabaya baada ya kipindi cha kwanza**

Yanga imefunga mabao 10 mpaka sasa hadi kufikia raundi ya pili, lakini manane kati ya hayo imeyapata kipindi cha pili. Imefunga mabao mawili tu kipindi cha kwanza na kuwa timu inayoongoza kwa kufunga mabao mengi kipindi cha pili.

Pia imefunga mabao manne kwenye kila mechi moja, ikianza dhidi ya KMC Agosti 23, mwaka huu katika Uwanja wa Azam Complex, ikiitwanga 5-0, yaliyopachikwa nyavuni dakika ya 58 na Stephane Aziz Ki, Hafiz Konkoni (dk. 69), Mudathr Yahaya (dk. 75) na Pacome Zouzoua (dk. 80). Ni bao moja tu lilifungwa kipindi cha kwanza na Dickson Job dakika ya 16.

Mechi ya pili ilicheza Agosti 29, ikiibamiza JKT Tanzania mabao 5-0, yaliyowekwa kwenye kamba dakika ya 54 na Kennedy Musonda, Yao Kouasi (dk. 64) na Maxi Nzengeli (dk. 79 na 88).

Stephane Aziz Ki alifunga bao pekee kipindi cha kwanza dakika ya 45.

**Azam noma kipindi cha kwanza**

Azam ndiyo timu inayoongoza kwa kufunga mabao mengi kipindi cha kwanza. Katika mabao saba iliyofunga mpaka sasa, matano imeyatumbukiza kipindi hicho.

Agosti 16, kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam, iliibamiza Kitayosce 4-0, yote yakifungwa kipindi cha kwanza na Feisal Salum kwa 'hat-trick' dakika ya tatu, tisa na 12, na moja la Prince Dube (dk. 5).

Agosti 28, mwaka huu katika uwanja huo huo, iliishindilia Prisons mabao 3-1, moja likifungwa kipindi cha kwanza na Dube dakika ya 11 likifanya idadi ya mabao ya kipindi cha kwanza kufikia matano, mawili yaliyofuata yakifungwa kipindi cha pili na Idd Selemani 'Nado' na Nathaniel Chilambo.

**Yanga, Azam pointi sita nyumbani**

Timu za Yanga na Azam zimeshinda mechi zao zote mbili zikicheza viwanja vyao vya nyumbani. Timu hizo zinatumia Uwanja wa Azam Complex kama wao wa nyumbani na zimevuna pointi sita mpaka sasa.

**Namungo penalti ya kwanza**

Katika mechi 16 zilizochezwa ni penalti moja pekee iliyopatikana, Namungo FC ikibahatika kuipata na kuikwamisha wavuni Agosti 19, mwaka huu kwenye Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa Lindi katika mechi iliyocheza dhidi ya KMC na kuwa penalti ya kwanza msimu huu kupatikana.

Mchezaji Fabrice Ngoye ndiye aliyefunga penalti hiyo na kuifanya timu yake ya Namungo kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya KMC.

**Kagera pekee haina ponti**


Timu ya Kagera Sugar ndiyo timu pekee ambayo haina pointi yoyote mpaka sasa, ikipoteza mechi zake zote mbili ambazo imecheza. Ilianza kwa kuchapwa mabao 2-0 dhidi ya Mashujaa FC, Agosti 16, kabla ya kufungwa bao 1-0 dhidi ya Ihefu, Agosti 19, mwaka huu.

**Singida, Kagera, Kitayosce hazina mabao**

Mpaka sasa timu za Singida Fountain Gate, Kitayosce na Kagera Sugar hazijafunga bao lolote hadi kufikia raundi ya pili.

Singida imetoka suluhu mechi zote mbili dhidi ya Prisons na Kitayosce, Kagera ikafungwa mabao 2-0 dhidi ya Mashujaa na bao 1-0 dhidi ya Ihefu na Kitayosce ilifungwa mabao 4-0 dhidi ya Azam na suluhu dhidi ya Singida.

**JE, WAJUA?**



KIPIGO cha mabao 7-0, Atletico Madrid ilichokitoa kwa Rayo Vallecano kwenye La Liga Jumatatu iliyopita, ni ushindi mkubwa wa pili kuwahi kuupata katika historia yake kwenye ligi hiyo baada ya kutoa adhabu kama hiyo dhidi ya Getafe mwaka 2013.





# Wazazi kitanzini mmomonyoko wa maadili kwa watoto

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KUKITHIRI kwa vitendo vya mmomonyoko wa maadili nchini wazazi wametakiwa kuwalinda watoto wao ili wasiharibiwe na tamaduni za kigeni, ikiwamo kujihusisha na vitendo vya ndoa za jinsia moja.

Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Dodoma, Pilly Mbaga, alitoa rai hiyo juzi kwenye mahafali ya kwanza ya darasa la saba Shule ya Awali na Msingi ya East Africa ya jijini hapa.

Mbaga alisema hivi sasa dunia imeharibika sana, hivyo wazazi wanawajibu wa kuhakikisha wanawalinda watoto wao ili wasiharibiwe na tamaduni za mataifa mengine.

"Hivi sasa ndugu zangu dunia imeharibika sana vitendo vya mmomonyoko wa maadili vimekithiri sana, hivyo wazazi mnapaswa kuwalinda watoto ili wasiharibiwe na tamaduni za mataifa mengi.

"Mataifa ambayo yamekuwa yakihamasisha masuala ya ndoa za jinsia moja na mambo mengine ambayo ni kunyume ya tamaduni za kitanzania na ni kinyume na mpango wa Mungu yamekuwa yakitumia mbinu mbalimbali kufanikisha jambo lao," alisema Mbaga.

Aidha, aliwataka wazazi kuacha tabia ya kutelekeza suala la malezi ya watoto kwa walimu pekee yao bali wanapaswa kuwasimamia na kuwafuatilia kila wakati ili wabaini vikwazo ambayo wanakabiliwa navyo.

"Wazazi hatupaswi kuacha suala la malezi kwa walimu pekee yao bali tuhakikishe kuwa tunawafuatilia watoto wetu kwa kushirikiana na walimu ili kuwasaidia wasiingie kwenye mikono ya shetani hali ibadilika sana hivi sasa watoto wamekuwa na tabia za ajabu ambazo kama hatutakuwa makini nao tutawapoteza," alisema.

Kadhalika, aliwataka walimu kuhakikisha kuwa wanasimamia watoto hasa wanapokuwa katika mabweni ili kubaini kama kuna mabadiliko yoyote ya kitabia na kuchukua hatua mapema kabla ya kundi kubwa kuharibiwa.

Vile vile, aliipongeza shule hiyo kwa kuunga mkono wa jitihada za serika katika uwekezaji kwenye sekta ya elimu ili kutoa elimu bora kwa watoto wa Kitanzania.

"Mkurugenzi niwapongeze sana kwa uwekezaji huu katika sekta ya elimu sisi chama pamoja na serikali kwa ujumla tutaendelea kutoa ushirikinao kwenu ili mfikie malengo yenu," alisema.

Alisema azma ya serikali ya awamu ya sita ni kuboresha elimu ambapo hivi sasa imefanya uwekezaji mkubwa katika ujenzi wa madarasa, maabara, mabweni pamoja na miundombinu mingine ili kuinua kiwango cha elimu nchini.

Awali Mkurugenzi wa shule hiyo, Dk. Rose Rwakatare, aliishukuru serikali kwa kuendelea kuweka mazingira rafiki kwa wawekezaji wazawa.

"Serikali ilipohamia hapa wakati wa hayati Rais Magufuli alitoa wito kwa wawekezaji kuwekeza miundombinu mbalimbali ili kusaidia kutoa elimu na sisi kama watua mabo tumebobea katika elimu tuliamua kuwekeza kwa kujenga shule hii ili kuweza kutoa elimu bora," alisema.

Hata hivyo, alisema lengo la shule hiyo ni kuunga mkono jitihada za serikali katika utoaji wa elimu bora kwa watoto wa kitanzania ili kuwawezesha kutoa ushindani katika soko la ajira duniani.



Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya TEHAMA, Dk. Nkundwe Mwasaga, akizungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa majukumu ya tume hiyo na mwelekeo wa utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2023/24 jijini Dodoma jana, kwenye ukumbi wa Idara ya Habari **(MAELEZO). PICHA: PAUL MABEJA**

# 'Kuunganisha mifuko hifadhi jamii kumepunguza gharama uendeshaji'

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

BUNGE limeelezwa kuwa hatua ya serikali ya kuunganisha mifuko ya hifadhi ya jamii imepunguza gharama za uendeshaji kutoka asilimia 12 hadi tano kwa Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSSSF).

Aidha, thamani ya mfuko huo imeongezeka kutoka Sh.trilioni tano hadi 8.1.

Naibu Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akijibu maswali ya nyongeza ya Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Nancy Nyalusi.

Katika maswali yake, Mbunge huyo alihoji ni hatua gani za serikali limechukuliwa ili kuondoa usumbufu kwa wanachama kupata mafao yao na kwamba kuunganisha mifuko ya pensheni (GEPF, LAPF, PPF na PSPF) haioni imechangia kuzaa vikwazo.

Akijibu maswali hayo, Katambi alisema mifuko ya pensheni ilikuwa mingi hali iliyosababisha kuwapo gharama kubwa za uendeshaji na serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan imepunguza gharama hizo.

"Mifuko iliunganishwa sababu kulikuwa na changamoto ya uwiano wa mafao sababu unakuta watu walikuwa mifuko tofauti wamestaafu kwa pamoja na kutumikia taifa sawa lakini mmoja analipwa Sh.milioni 40, mwingine Sh. milioni 75 kwa sababu ya utofauti wa mifuko." "Kwa hiyo kutengeneza ulinganifu tukaona tuunganishe mifuko ili kuweka uwiano sawa wa kiwango cha malipo kwa mujibu wa utafiti uliofanyika na kubaini viwango hivyo kuwa tofauti," alisema.

Alitaja sababu nyingine ya kuunganishwa mifuko ilikuwa mingi na ilisuasua kujisimamia. Katambi alisema mifuko ya PSSSF na NSSF(Mfuko wa Hifadhi ya Jamii) imeondoa kero kwa wastaafu na kulipa mafao kwa wakati. "Tunalipa ndani ya siku 60 kama mfanyakazi hakuna changamoto zozote za kitaarifa au kumbukumbu au hata wakati mwingine ndani au chini ya siku saba."

"Hatua nyingine ambayo serikali imechukua kupunguza usumbufu imefanya ni kuweka mfumo wa TEHAMA mwanachama kupata taarifa kupitia simu ya kiganjani na hatua nyingine pia ni kuunganisha mifuko kutengeneza utaratibu wa uwiano katika malipo lakini pia ulinganifu,"alisema.

Awali, katika swali lake la msingi, Mbunge huyo alihoji lini serikali itaboresha mafao ya wastaafu kwa kuongeza kiwango cha pensheni anayopata mstaafu kwa mwezi.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Katambi alisema hadi sasa wastaafu wote wa serikali wameboreshewa pensheni zao za kila mwezi ambapo kiwango cha chini ni Sh. 100,000 na kuendelea tofauti na hapo awali.

Alisema Mifuko ya Hifadhi ya Jamii huongeza kiwango cha pensheni ya kila mwezi kwa wastaafu baada ya kufanya tathmini na kujua uendelevu wake na uwezo wa kulipa mafao kwa wanachama wake.

# Kampuni upimaji ardhi zaonywa kuhusu gharama kubwa

**Na Thobias Mwanakatwe,**

KAMISHNA wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Singida, Shamim Hoza, ametoa onyo kwa kampuni za upimaji ardhi mkoani hapa kuhakikisha yanatoza bei elekezi iliyopangwa na serikali wakati wa upimaji.

Amesema kinyume na hapo yatachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwamo kufutiwa kibali cha kufanya kazi hiyo.

Alitoa maagizo hayo juzi katika kikao kazi cha watumishi wa sekta ya ardhi na kueleza kwamba kampuni zinazojishughulisha na upimaji ardhi zisijiingize kutoza fedha nyingi kinyume na maelekezo ya serikali.

Hoza alisema lengo la serikali kushirikiana na taasisi na kampuni binafsi ni kusogeza huduma na kuhakikisha wananchi wanazipa kwa urahisi, hivyo haiwezi kuvumilia kuona wananchi wake wakifanyiwa ndivyo sivyo.

Aidha, Hoza aliwaomba wakurugenzi wa halmashauri za wilaya na manispaa kushirikiana na kampuni hizo na kuwa uwezo wa serikali.

Naye Ofisa Ardhi Wilaya ya Manyoni, Pendo Mwakila, alisema lengo la kikao hicho ni kuwataka maofisa ardhi kutoka ofisini na kuwafuata wananchi waliko ili kusikiliza kero zao ili kuwapunguzia gharama za kuwafuata maofisini na kuwa wao walikwisha anza katika Kata ya Kintiku na Kilimatinde. Ofisa wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), mkoani hapa, Shemu Mgaya alizungumzia kuhusu maadili ya utumishi wa umma na watumishi wakiwamo wa sekta ya ardhi kutojihusisha na rushwa katika utendaji wa kazi zao.

Naye Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi Wilaya ya Singida, Bahati Colex aliwaomba maofisa ardhi kushirikiana na wananchi wanaoshinda kesi kurudishiwa maeneo yao, kwani imekuwapo changamoto kubwa kutoka kwa maofisa hao ya kuwazungusha pasipo sababu yoyote licha ya kushinda kesi hizo.

Msajili Hati Msaidizi Mkoa wa Singida, Palmon Rwegoshora, alisema lengo lingine la kikao kazi hicho ni kuwahamasisha maofisa ardhi kwenda kwa wananchi kuwaeleza gharama za umilikishaji zimepungua kutoka na punguzo lililotolewa na serikali ambalo ni nusu bei ya gharama za awali.

Alisema kutokana na punguzo hilo wanategemea watu wengi watamilikishwa viwanja vyao na kupata hati na kwenda kwenye taasisi za kifedha kukopa.

Mpima Ardhi Mkoa wa Singida, Sesaria Williams, ameungana na serikali kwa uamuzi iliochukua ya kutoa punguzo hilo ambapo awali maombi ya umilikishwaji yalikuwa Sh. 50,000 lakini sasa ni Sh. 25,000 na ada ya ramani ndogo ya hati ilikuwa Sh. 20,000 lakini sasa ni bure.

Awali maombi ya kumilikishwa ilikuwa ni Sh. 20,000 ambapo sasa ni Sh.5,000.

Mratibu wa Kodi ya Ardhi Mkoa wa Singida, Benedict Mombeki alisema kodi ya pango la ardhi mkoani hapa bado kuna mwitikio mdogo zaidi au wananchi wanauchumi wa chini na wanailipa kwa kusuasua.





## Kikongwe matatani tuhuma kumuua mjukuu kwa jembe

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, linamshikilia Malogi Luobela (75) mkazi wa Kijiji cha Ikoho Wilaya ya Mbeya kwa tuhuma za kumuua mjukuu wake aitwaye Vision Erick (mwaka mmoja na miezi mitano) kwa kumkata kwa jembe kichwani.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Benjamin Kuzaga, alisema tukio hilo lilitokea Agosti 31 saa 4:30 asubuhi nyumbani kwa bibi huyo.

Alisema chanzo cha tukio hilo ni kwamba mtuhumiwa alikuwa anachimba udongo ili 'kukandika' (kusiriba) nyumba na wakati anaendelea mtoto huyu alitambaa hadi eneo hilo bila mtuhumiwa kumuona na ndipo akamkata na kusababisha kifo.

Kamanda Kuzaga alisema bibi kizee huyo ana tatizo la upofu wa macho na kwamba ndiyo sababu ilimfanya asimuone mtoto huyo wakati anachimba udongo.

"Mtuhumiwa tunaendelea kumshikilia kwa ajili ya hatua za kisheria, lakini nitowe wito kwa mabinti kuacha tabia ya kuwaachia wazee watoto na wao kwenda kwenye shughuli zao za kujipatia kipato," alisema Kamanda Kuzaga.

Katika hatua nyingine Kamanda Kuzaga alisema jeshi hilo linamsaka dereva wa gari yenye namba za usajili T.436 CGD aina ya Mitsubishi Canter mali ya Kampuni ya Mainland Pharmacy Center aitwaye Kadhar Adamu (28) mkazi wa Mkoa wa Katavi kwa tuhuma za kumgonga kwa makusudi askari wa usalama barabarani.

Alisema kijana huyo alimgonga askari wa kikosi cha usalama barabarani WP.2645 S/SGT Zaina akiwa kwenye majukumu yake katika eneo la Kabwe Barabara Kuu ya Mbeya-Njombe kisha akatelekeza gari na kukimbia.

Alisema chanzo cha ajali hiyo ni uzembe wa dereva huyo mwenye asili ya Somalia ambaye alikuwa anaendesha gari kwa mwendo mkali bila kuzingatia kuwa eneo hilo ni lenye msongamano wa watu na kwamba ilikuwa ni kwenye eneo la kivuko cha watembea kwa miguu.

"Askari huyo aliumia maeneo mbalimbali ya mwili wake ikiwamo kiuno, mgongo na kichwani na anaendelea kupata matibabu katika Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya, kwa sasa anaendelea vizuri, nitumie nafasi hii kumtaka dereva huyo ajitokeze," alisema Kamanda Kuzaga.

Alisema wanaendelea kufuatilia katika maeneo mbalimbali ili kubaini alipo dereva huyo ili akamatwe na achukuliwe hatua za kisheria.

## Makada CHADEMA walioshiriki uchaguzi Mbarali matatani

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kanda ya Nyasa, kimeanza kuwachukulia hatua baadhi ya wanachama wake wakiwamo viongozi kwa tuhuma za kukiuka katazo la kutoshiriki uchaguzi mdogo wa ubunge Mbarali mkoani Mbeya.

Wanachama hao wanadaiwa kushiriki harakati za uchaguzi huo kwa kuwanadi wagombea wa vyama vingine vya upinzani ambavyo vinashiriki uchaguzi huo jambo ambalo walizuiwa.

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu wa CHADEMA Kanda ya Nyasa, Gwamaka Mbughi, alisema chama hicho kilishaweka msimamo wake kwamba hakitashiriki uchaguzi wa aina yoyote bila Tume ya Taifa ya Uchaguzi kurekebishwa.

Alisema kutokana na msimamo huo, walitoa maelekezo kwa wanachama na viongozi wa chama hicho Wilaya ya Mbarali kutoshiriki kwa namna yoyote uchaguzi mdogo wa ubunge unaoendelea.

Alisema pamoja na katazo hilo lakini baadhi ya viongozi waliamua kushiriki kwa kupanda majukwaani na kuwanadi wagombea wa baadhi ya vyama ili kufanikisha ushindi wao.Mbughi alisema viongozi waliochukuliwa hatua wapo wanne ambao Diwani wa Kata ya Ubaruku, Alex Kiswaga na viongozi watatu wa kata mbalimbali za Wilaya ya Mbarali.

Alisema kati ya viongozi hao ni diwani pekee ndiye anashughulikiwa na mamlaka ya nidhamu ya mkoa lakini viongozi wa kata wanashughulikiwa na mamlaka ya nidhamu ya Wilaya ya Mbarali.

"Tulishawapa maelekezo ya kutoshiriki uchaguzi huo, lakini wao wamekiuka kwa kurubuniwa na viongozi wa vyama hivyo ambao wanataka kutumia mtandao wetu kufanikisha ushindi wao, tumewaandikia barua za kuwataka wajieleze," alisema Gwamaka.

Aliwatahadharisha wanachama wengine wa chama hicho kutothubutu kwa namna yoyote kushiriki uchaguzi huo kwa maelezo kuwa watachukuliwa hatua kali za kinidhamu.

Hata hivyo alisema chama hicho hakitashiriki pia uchaguzi mdogo wa moja ya kata za mkoani Rukwa ambayo diwani aliyekuwa wa chama hicho alifariki.

Katika hatua nyingine Mbughi aliwataka wanachama wa chama hicho kujiandaa na Operesheni +255 ambayo inaendelea nchi nzima kwa maelezo kuwa itafanyika katika Kanda ya Nyasa baada ya kuhitimishwa katika Kanda ya Serengeti ambako inaendelea kwa sasa.

Alisema operesheni hiyo itahitimishwa katika Kanda ya Serengeti Septemba 17 mwaka huu na baada ya hapo kutakuwa na mapumziko na tathmini kabla ya kuhamia katika kanda hiyo ya Nyasa.

"Operesheni hiyo itaambatana na usajili wa wanachama kielektroniki na kutoa elimu kuhusu mambo mbalimbali ya kitaifa, kwahiyo tunawahamasisha wanachama wetu wajiandae," alisema Mbughi.

Diwani Kiswaga ndiye diwani pekee wa CHADEMA aliyeshinda kwenye Uchaguzi Mkuu wa 2020 katika Jimbo la Mbarali na kata zingine zote walishinda madiwani wa Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Aidha, uchaguzi mdogo unafanyika Mbarali kwa ajili ya kuziba pengo lililoachwa na aliyekuwa mbuge wa jimbo hilo, Francis Mtega ambaye alifariki kwa kugongwa na trekta dogo (Power tiller) alipokuwa anaendesha pikipiki kuelekea shambani.



Meneja Masoko wa Kampuni ya BetPawa Tanzania, Borah Ndanyungu (kushoto), akiwa pamoja na SP Deus Sokoni, Mkuu wa Dawati la Elimu, Kitengo cha Usalama Barabarani kutoka Jeshi la Polisi, wakimkabidhi cheti Boniface Matale mmoja kati ya madereva bodaboda 250 aliyeshiriki mafunzo ya usalama barabarani kwa Mkoa wa Dar es Salaam. Mfunzo hayo yalidhaminiwa na BetPawa kushirikiana na Jeshi la Polisi Kitengo cha Usalama Barabarani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Uuzaji mazao shambani chanzo Tanzania kukosa ushindani

**Elizabeth John,** NJOMBE

IMEELEZWA kuwa baadhi ya wakulima wa mikoa ya Njombe na Ruvuma wamekuwa wakiwauzia wafanyabiashara wa kigeni mazao yakiwa shambani jambo ambalo linasababisha Tanzania kukosa ushindani na kibiashara kwenye soko huru la Afrika.

Tatizo hilo lilielezwa na Ofisa Biashara Mkuu Kutoka TAN TRADE, Crispin Luanda, wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya mafunzo kwa wafanyabiashara yaliyofanyika mkoani hapa mwishoni mwa wiki.

Alisema wanaendelea kuhamasisha Watanzania hususani wafanyabiashara kutumia soko huru la afrika akisisitiza kuwa Tanzania imeingia makubaliano na nchi nyingine Afrika kuwafanya wananchi wawe huru kufanya biashara kwenye nchi hizo.

Alisema kuwa pamoja na kuhamasisha wananchi kwenda kufanya biashara nchi nyingine pia wapo wananchi wa nchi nyingine ambao wanaingia nchini kufanya biashara bila ya kufuata taratibu.

"Kwa hiyo tatizo tulilolibaini kwa mikoa ya Njombe na Ruvuma ni kwamba wafanyabiashara wa nchi nyingine wanapokuja nchini wanakwenda mpaka mashambani kununua bidhaa huko, sasa hili ni tatizo ambalo tunasisitiza lidhibitiwe," alisema Luanda.

Luanda alisema madhara ya kuwapeleka watu mashambani ni pamoja na kukosekana suala zima la udhibiti wa ubora, ushuru wa serikali kwa mtu anayetoka nje kuulipa sambamba na ushindani wa kibiashara. Ezekiel Richard ni msafirishaji wa zao la parachichi kutoka Kampuni ya Highland Organic aliishauri serikali kupunguza vikwazo kwa wafanyabiashara wa mali mbichi ikiwemo matunda kwa sababu uwepo wa milolongo unasababisha bidhaa kuharibika kabla hazijafika sokoni.

"Kuna changamoto ya kiutawala mfano bandari lakini pia kwenye Aiport nilikuwa natamani tusaidiwe kupunguza ule mlolongo wa kucheleweshwa mizigo haswa hii ya matunda yanayoharibika kwa hiyo yanapochelewa kunakuwa na changamoto ya kuharibika na kuendelea kupoteza soko kwa hiyo pia tunatamani baadhi ya vitengo tuviamishie mikoani ili kurahisisha kupoteza muda unapofika bandarini na mzigo," alisema Richard.

Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Njombe, Edward Mwakipesile, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwa na mkakati wa kutumia fursa za kimasoko zilizopo katika eneo huru la biashara barani Afrika kwa kuwa bidhaa na huduma zinazozalishwa nchini zimatakiwa kufika katika soko huru barani Afrika. "Lakini tumepata namna ya kuboresha bidhaa zinazozalishwa ili kukabiliana na ushindani uliopo katika soko huru la Afrika pamoja na kuongezeka idadi ya namba za bidhaa zinazozalishwa ili kupata kufahamika na vile vile kumiliki soko husika," alisema Mwakipesile.

Mwenyekiti wa Chemba ya Wafanyabiashara Wenye Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA) Mkoa wa Njombe, Bernad Mlyuka, aliiomba serikali hasa maofisa biashara na watendaji kwamba wawe makini katika kutoa vibali.



## Umoja wa Wanawake CCM watakiwa kukemea makundi

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

WATENDAJI na viongozi wa Umoja wa Wanawake wa CCM Zanzibar wametakiwa kuwafuatilia wanachama wanaoendeleza makundi ili kuwafikisha katika kamati za maadili za chama hicho ili kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

Ushauri huo umetolewa na Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT ) Ofisi ya Zanzibar, Tunu Juma Kondo wakati akifungua mafunzo elekezi kwa watendaji na viongozi wa UWT Mkoa wa Magharibi Unguja kichama uliofanyika katika ukumbi wa CCM Kiembesamaki.

Alisema viongozi wa CCM wameshachaguliwa katika uchaguzi uliopita, hivyo wanatakiwa kushirikiana nao ili waweze kuwaletea maendeleo.

Alisema kuwa UWT haitomvumilia mtu yeyote atakayebainika kubeba wagombea na hawatosita kumwondosha katika nafasi yake.

Aidha, aliwataka kuyafanyia kazi kwa vitendo mafunzo waliopewa ili yaweze kuleta tija katika chama na taifa kwa ujumla.

Tunu aliwataka kuwasilisha matatizo ya wanawake wenzao katika vikao halali ili kuondosha majungu, fitina na uhasama miongoni mwao.

Akiwasilisha mada ya udhalilishaji wa kijinsia, Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Siti Abasi Ali, aliwataka wazazi na walezi kuwa makini katika malezi ya watoto na kuacha kutoa talaka kiholela ili kuondosha vitendo vya udhalilishaji kwa watoto wao.

Pia aliwataka wanaume kutowaachia mzigo mkubwa wa malezi wanawake ili kuwalinda na kuwakinga na vitendo vya udhalilishaji watoto wao.

Kadhalika aliwataka wanaume kuwaachia wake zao kufanya biashara halali ili kusaidiana kimaisha na kupata kipato cha kuendesha maisha yao.

Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Mkoa wa Magharibi kichama, Fatma Ali Ameir alisema lengo la kuandaa mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo watendaji na viongozi ili kubadilika na kufanya kazi kwa ufanisi na kuepukana na kufanya kazi kwa mazoea.

# DC ataka elimu zaidi kukabiliana afya ya akili

**Na Beatrice Shayo**

SERIKALI imesema ipo haja ya wananchi kupatiwa elimu ili kujikinga na maradhi yanayosababishwa na tatizo la afya ya akili.

Wito huo umetolewa mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam na Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo, alipomwakilisha Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tanzania Bara, Kanali Mstaafu, Abdulrahman Kinana wakati wa usiku wa afya ya akili kinga iliyoandaliwa na Family Vibes Foundation na Jumuiya ya Maridhiano na Amani Tanzania.

Mpogolo alisema taasisi hiyo inatamani kuona kila Mtanzania anakuwa na afya njema, ndiyo maana wameamua kuchangisha fedha ili kuhakikisha inapeleka elimu kwa wananchi.

"Wana jambo jema utafiti zimefanyika kuona namna gani na afya ya akili ina mahusiano kwa binadamu, Shirika la Afya Duniani (WHO) mwaka 2017, iliangalia eneo moja la wafanyakazi na kubaini asilimia 10 ya wafanyakazi wanachangamoto ya afya ya akili," alisema Mpogolo na kuongeza:

"Unaweza ukarudisha nyuma akili yako embu tazama ofisini kwako ni wangapi ambao ni marafiki zako utasikia nimegombana na mume wangu, mambo yangu hayaendi mara mama anahitaji fedha ni wangapi wanaeleza hayo."

Mpogolo alisema zaidi ya asilimia 10 ya wafanyakazi wanatumia muda wa kazi kutibu shughuli za afya ya akili, anaweza mtu amefika ofisini anashindwa kufanya kazi kutokana na msongo wa mawazo ya nyumbani kwake.

Mpogolo alisema Jumuiya ya Kimataifa ikiwamo na Tanzania ziliridhia na kuweka azimio ifikapo mwaka 2030 kuhakikisha wanatatua changamoto za afya ya akili, hivyo kinachofanyika ni malengo kwa nchi zote duniani kuhakikisha zinapambana na afya ya akili.

Alisema ni muhimu kuwaelimisha wananchi kwa sababu maisha ya wanadamu yanashuka na kupanda hivyo wanapoelimishwa itawasaidia kupunguza madhara.

Alisema zipo changamoto za maisha ambapo watu wanaona mambo yao hayaendi na wengine kuona suluhu ni kujiua kumbe anasumbuliwa na afya ya akili.

Mkurugenzi wa Family Vibes Foundation, Dk. Maryrose Kajinge alisema jambo la msingi katika kuzingatia afya ya akili ni kuwa na uvumilivu na kufanya maamuzi sahihi na kuepuka kubeba chuki za muda mrefu katika maisha.

"Hautakiwi kubeba mambo mabaya kichwani hakuna ugonjwa hatari kama hili linaloenea kwa kasi kama chuki, siyo kila ugonjwa ni maradhi," alifafanua.

Alisema mtu anaposhindwa kumsamehe mwingine ana shida katika afya ya akili hata wakati mwingine hujikuta unashindwa kufanya kazi.



Mbunge wa Kojani ambaye ni Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Hamad Hassan Chande (katikati), akiwa pamoja na Meneja wa Tanzania Commercial Bank (TCB) Pemba, Shomary Rimisho, baada ya kupokea msaada wa vyerehani 20 vya kisasa vilivyotolewa na TCB kwa ajili ya kusaidia kinamama visiwani Unguja. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Uhaba wa vipimo vya kupima VVU waikumba Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KWA muda wa miezi mitatu Zanzibar inakabiliwa na uhaba wa kifaa cha uchunguzi wa Virusi Vya Ukimwi (VVU) katika vituo vya afya vya serikali hali ambayo imesababisha huduma ya upimaji wa VVU kudorora.

Wakizungumza na waandishi wa habari, kwa nyakati tofauti walipotembelea vituo hivyo, wataalamu wa afya katika Kituo cha Afya Fuoni, Tunguu, Mwera, Magirisi pamoja na vituo rafiki, walisema kuwa wananchi hasa vijana wamehamasika kupima VVU na hufika kwa wingi kupata huduma hiyo, lakini kutokana na uhaba wa kifaa hicho huduma hiyo ilikuwa na kusuasua.

Daktari wa Kituo cha Afya Fuoni, Sultani Shela, alisema tatizo hilo la uhaba wa kifaa hicho cha uchunguzi ni zaidi ya miezi miwili, kwamba havipatikani katika vituo vya huduma rafiki kwa vijana pamoja na vituo vya afya.

Alisema hali hiyo imesababisha watu kwenda katika hospitali binafsi ambapo huduma hiyo hutolewa kwa gharama ya malipo.

Alisema huduma hiyo hupatikana kwa wajawazito pekee kituoni hapo kwa sababu vifaa walivyonavyo ni vichache na mjamzito kabla ya kujifungua lazima kujua afya yake ili kumkinga mtoto na maambukizi.

"Vituo vyote vya serikali huduma ya upimaji wa HIV ni bure na ndiyo maana wananchi hufika kwa wingi kwa ajili ya kujua afya zao," alisema Khadija Ali Khamis wa Kituo cha Mwera.

Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, alikiri uwapo wa uhaba wa kifaa hicho akisema tatizo hilo limetokana na kuchelewa kwa kufika kontena lenye vifaa hivyo kutoka nje ya nchi.

Aidha, alisema tayari kontena hilo imeshafika na leo (Jumatatu) vifaa hivyo vitaanza kusambazwa katika vituo vyote vya afya vya serikali ili kuendelea kutoa huduma hiyo ya uchunguzi ya HIV. Alisema serikali inapata msaada wa vifaa hivyo kutoka Global Fund na vifaa vilivyofika vitakidhi mahitaji kwa muda wa mwaka mmoja.

Hivyo, aliwataka wananchi kuendelea kuvitumia vituo vya afya na vituo vya huduma rafiki kwa ajili ya kupata huduma mbalimbali za kiafya ikiwemo uchunguzi wa HIV, ambapo maambukizi yake kwa sasa yapo katika makundi maalum ikiwamo vijana wanaotumia dawa za kulevya na wanaofanya biashara ya ngono.

Ziara hiyo ya waandishi wa habari imeandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (TAMWA) kupitia mradi wa afya ya uzazi ambao unaendeshwa na chama hicho.

# Wataalamu watakiwa kuelimisha wakulima utabiri mvua ya vuli

**Na Renatha Msungu**

WIZARA ya Kilimo imewataka maofisa ugani kusambaza kwa wakulima, utabiri wa mwelekeo wa mvua ya vuli, inayotarajia kuanza Oktoba hadi Desemba, mwaka huu, iliyotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Nchini (TMA), ili kuepuka athari za uharibifu wa mimea, ikiwamo kupanda mazao yanayoendana na hali hiyo.

Serikali imewataka wakulima kupanda mazao yanayostahimili unyevu kwa kuzingatia kanuni za kilimo kutoka kwa wataalamu wa kilimo, huku ikisisitiza kupanda zao la mpunga linalostahimili hali ya unyevu.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Gerald Mweli, alibainisha hayo katika taarifa yake kuhusu hali ya mwelekeo wa mvua ya vuli, iliotolewa na TMA ambayo inaigusa mikoa mbalimbali nchini.

Taarifa hiyo inaonyesha kuwa, mvua ya vuli inatarajiwa kuanza Oktoba hadi Desemba katika maeneo yanayopata mvua kwa misimu miwili kwa mwaka, maeneo hayo yanajumuisha mikoa ya Nyanda za Juu Kaskazini, Mashariki, Kanda ya Ziwa Victoria na Kanda ya Pwani Kaskazini.

Katibu Mweli alisema kwa mujibu wa taarifa hiyo mvua itakuwa juu ya wastani hadi wastani katika maeneo mengi ya mikoa ya Kigoma, Dar es Salaam, Tanga, Pwani, Simiyu, ikiwamo visiwani vya Mafia na kaskazini mwa mikoa ya Morogoro, inatarajia kuanza wiki ya nne ya mwezi Septemba.

Alisema katika maeneo ya Magharibi ya Ziwa ya Victoria na kusambaa katika maeneo mengine mvua hiyo inatarajia kuanza mwezi Oktoba.

Alisema mvua ya wastani hadi juu ya wastani inatarajiwa kunyesha katika mikoa ya Mara kaskazini mwa mikoa ya Simiyu, Arusha, Manyara na Kilimanjaro kuanzia wiki ya pili ya mwezi Oktoba.

Hata hivyo, alisema mvua hiyo inatarajia kunyenda hadi Januari, mwakani tofauti na kawaida na athari kadhaa zinaweza kujitokeza, kama mafuriko, milipuko ya magonjwa ya mimea na uharibifu wa miundombonu ya kilimo.

Wizara ya Kilimo imewashauri wakulima na wadau wengine wa sekta ya kilimo kuchukua hatua mbalimbali zikiwamo kuandaa mashamba mapema, kununua pembejeo, mbegu na viuatilifu pamoja na mahitaji muhimu ya kilimo kabla ya kuanza kwa mvua.

Pia wakulima wanapaswa kutumia mvua hiyo kupanda mazao yanayohimili viwango vikubwa vya unyevu ardhini kama mpunga, kwa kuzingatia kanuni za kilimo ikiwamo kupanda kwa wakati.

Alifafanua kuwa, wataalamu wa kilimo, maofisa ugani wanapaswa kufuatilia, kutafsiri na kusambaza kwa wakulima taarifa ya hali ya hewa iliyotangazwa na TMA ili uzalishaji ufanyike kwa tija na kupunguza athari mbalimbali.

Katibu Mweli aliwaasa wakulima na wadau wengine kuimarisha mifereji, huku wataalamu wa kilimo katika ngazi za halmashauri, kata na wilaya, kushirikiana na wakulima kuandaa kalenda maalum za uzalishaji wa mazao ili kuepuka athari.

Aidha Wizara ya Kilimo, imewasisitiza wakulima, kukarabati miundombinu ya kuhifadhi chakula, kulima kilimo kinachozingatia kanuni pamoja na kushirikiana na wataalam wa sekta ya kilimo, ikiwamo kuzingatia matumizi ya makinga maji na kuimarisha miundombinu ya uvunaji.



Meneja Mauzo wa Kampuni ya The Squid Zanzibar Ltd anayeshughulikia mradi wa hoteli ya Ocean Pearl, Gina Washington (wa pili kushoto), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, wakati Benki ya Absa ikitangaza ushirikiano wa mikopo ya nyumba unaoifanya visiwani Zanzibar. Wengine kutoka kushoto kwake ni, Mkuu wa Kitengo cha Wateja Maalumu wa Benki ya Absa, Thereza Majinge, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Squid, George Alexandru na Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi wa Absa, Ndabu Lilian Swere. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DC akataa wilaya yake kutajwa ubadhirifu

**Na Julieth Mkireri,** CHALINZE

MKUU wa Wilaya ya Bagamoyo, Halima Okash, amesema ma hapendi kuwa mfano kwa wilaya yake kutajwa kwenye ubadhirifu wa fedha na kutaka viongozi kuwa wasimamizi wa mapato na matumizi kwenye halmashauri zao.

Vilevile, amesema viongozi wanatakiwa kuacha tabia ya kushawishi wananchi kupinga miradi kwenye maeneo yao jambo ambalo sio jema na ni kati ya vitu vinavyorudisha nyuma maendeleo.

Okash aliyesema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akizungumza kwenye kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Chalinze, kuwa kipo kikwazo kwa baadhi ya viongozi kushawishi wananchi kupinga miradi.

"Tuache kuwa vishawishi vya migogoro ya ardhi, tumsaidie Rais kuiondoa, pia kuna changamoto baadhi ya viongozi kuwa vinara wa kushawisi wananchi kuipinga miradi kwenye maeneo yao hili si jambo jema," alisisitiza.

Mbunge wa Jimbo la Chalinze, Ridhiwani Kikwete, aliwakumbusha madiwani kusimamia miradi kwenye maeneo yao iweze kutekelezwa kwa kiwango kinachotakiwa.

Ridhiwani ambaye ni Naibu Waziri Wiziri Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, alisema halmashauri hiyo itaendelea kuyaekeleza wananchi wanayoyataka na madiwani wafanye ziara kwenye maeneo yao kuelezea miradi iliyotekelezeka.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Hassan Mwinyikondo alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwezesha upatikanaji fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya halmashauri hiyo na kupunguza kero za wananchi.

Akizungumzia miradi inayopelekwa kwa wananchi, aliomba wasimamizi kushirikiana na madiwani katika utekelezaji wake.

# Wakazi vijiji vinne walalamikia mifugo kuvamia mashamba

**Na Christina Haule,** MOROGORO

WAKAZI wa vijiji vinne vilivyopo Kata ya Tomondo, Tarafa ya Mikese wilayani Morogoro wamesema ni vyema serikali ikawaondolea kero ya mifugo vamizi kwenye maeneo yao inayoharibu mazao, miundombinu na vyanzo vya maji na kuwarudisha nyuma kimaendeleo.

Wakazi hao walitoa kilio hicho jana wakiwa kwenye warsha ya kujengewa uwezo masuala ya usawa wa kijinsia, haki za wanawake na stadi za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi iliyoandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP- Mtandao) na kufanyika kwenye kata hiyo na kwamba isipopata ufumbuzi ni rahisi kusababisha vurugu na hata mapigano.

Bashiri Kondo (26), mkazi wa Kijiji cha Kikundi, alisema suala la uvamizi wa mifugo wanaotoka kata za jirani ikiwamo Mlilingwa ni kero kubwa hasa vijana walioamua kujiajiri kulima mboga.

Aidha, wameiomba serikali ya wilaya kushirikiana na mkoa kuona umuhimu wa kutunga na kusimamia vifungu vya sheria vya kumfanya mwanamume kutumia fedha za mavuno ya kilimo kwa maslahi ya familia badala ya kuongeza mke wa pili.

Augenia Venance, alisema matumizi ya fedha za mavuno upande mmoja huchangia kudhorota kwa familia katika masuala ya maendeleo hasa kielimu kwa watoto kwa sababu ya wanaume kutolipa ada, kutonunua chakula nyumbani, vifaa vya shule vya watoto na pengine kutoroka kabisa majumbani mwao.

Alisema licha ya kuwepo kwa usawa wa kijinsia katika utendaji wa shughuli mbalimbali kwenye kata hiyo, bado wapo wanaume wanaowanyima haki ya usawa wa matumizi ya fedha za mali za pamoja wanawake na kusababisha kuombwa talaka na wanawake kwenda kuanza maisha kwingine huku wakiwaacha watoto mikononi mwa mwanaume asioweza kutunza.

Mwenyekiti wa Kituo cha maarifa cha TGNP- Mtandao, Mwanahawa Salehe, alisema suala la mifugo vamizi likitatuliwa itasaidia kuwaondoa kwenye migogoro isiyokwisha iliyosababisha kulipishwa Sh. 28,000 kwa watu 80 wakidaiwa kuua ng'ombe saba wa wafugaji walipokuwa wakiwazuia kuingia kwenye mazao yao licha ya wao kuwa ndio waathirika wakubwa wa kulishiwa mifugo kwenye mazao yao.

## HABARI KIMATAIFA

## Gabon yafungua mipaka siku tatu baada ya mapinduzi

**LIBREVILLE,** GABON

NCHI ya Gabon imetangaza rasmi kuifungua tena mipaka yake ikiwa ni siku tatu baada ya kuifunga wakati wa mapinduzi ya kijeshi yaliyomwondoa madarakani, Rais Ali Bongo.

Msemaji wa Jeshi la Gabon akinukuliwa kupitia Televisheni ya Taifa alisema mipaka ya bahari, nchi kavu na anga nchi hiyo imefunguliwa kwa sababu viongozi wa kijeshi wanataka kuheshimu utawala wa sheria, mahusiano mema na nchi jirani pamoja na mataifa yote duniani.

Kulingana na msemaji huyo wa jeshi, hatua hiyo pia imechukuliwa ili kuonesha wajibu wa nchi hiyo kwa Jumuiya ya Kimataifa.

Mapinduzi ya kijeshi yaliyofanyika nchini humo mwishoni mwa wiki chini ya Jenerali Oligui Nguema ni ya nane kwenye mataifa ya Magharibi na Kati mwa Afrika ndani ya miaka mitatu.

Hali hiyo imezua hofu kuhusu majeshi kufanya mapinduzi kote katika ukanda huo na kufuta maendeleo ya kidemokrasia yaliyofikiwa ndani ya miongo miwili iliyopita. **DW**

## Watu 43 wauawa katika maandamano nchini DRC

**GOMA,** DRC

UMOJA wa Mataifa (UN) umeagiza kufanyika kwa uchunguzi huru, baada ya watu 43 kuuawa mwishoni mwa wiki katika mapambano na maofisa wa usalama katika mji wa Goma Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC).

Tukio hilo lilitokea wakati wa maandamano dhidi ya Jeshi la Kulinda Amani la Umoja wa Mataifa, MONUSCO yaliyopangwa na dhehebu la Mesia Wazalendo.

Wakati wito huo ukitolewa, Mkuu wa Tume ya Umoja wa Mataifa nchini DRC MONUSCO, Bintou Keita, amesema anasikitishwa na mauaji yaliyotokea na kutaka njia ya mazungumzo kutumiwa kutatua mizozo.

Kufuatia mauaji hayo, mashirika ya kiraia na yale ya kutetea haki za binadamu kama Lucha yamelaani kilichotokea na kutaka kusimamishwa kazi kwa Gavana wa Kijeshi wa Kivu Kaskazini na Meya wa Goma.

Shirika la Human Rights Watch nalo limelaani hatua ya serikali kuzuia maandamano hayo na familia za waathiriwa kuruhusiwa kuona miili ya wapendwa wao, huku serikali jijini Kinshasa kupitia msemaji wake na Waziri wa Habari Patrick Muyaya ikiahidi kuchunguza kilichotokea. **RFI**

# Maelfu waandamana Niger kutaka Ufaransa iondoe vikosi

**NIAMEY,** NIGER

**Waandamanaji hao walionekana wakiwa wameshika mabango yanayosomeka; "Wanajeshi wa Ufaransa, ondokeni nchini mwetu."**

MAELFU ya wananchi wameandamana katika Mji Mkuu wa Niger, Niamey wakiitaka Ufaransa iviondoe vikosi vyake nchini humo, kama ilivyoamriwa na utawala wa kijeshi ulioingia madarakani baada ya mapinduzi Julai 26.

Waandamanaji hao walikusanyika karibu na kambi ya wanajeshi ya Ufaransa baada ya mashirika kadhaa ya kiraia kutoa wito wa maandamano dhidi ya wanajeshi wa Ufaransa nchini humo.

Waandamanaji hao walionekana wakiwa wameshika mabango yanayosomeka;

"Wanajeshi wa Ufaransa, ondokeni nchini mwetu."

Maandamano hayo yalizidi kuwa makubwa kutokana na waandamanaji wapya kuwasili- mchana na umati mkubwa uliokuwa katika makutano ya barabara karibu na kambi ya wanajeshi wa Ufaransa nje kidogo ya Mji wa Niamey.

Utawala wa kijeshi wa Niger, mwishoni mwa wiki uliituhumu Ufaransa kwa kuingilia masuala ya ndani ya nchi kwa kumuunga mkono Rais aliyepinduliwa, Mohamed Bazoum.

Rais huyo mshirika wa Ufaransa ambaye kuchaguliwa kwake kulileta matumaini ya utulivu katika taifa hilo alikamatwa na wajumbe wa kitengo chake cha ulinzi Julai 26. **DW**




Baadhi ya wananchi nchini Niger wakiwa wamebeba mabango, wengine wakiwa juu ya magari wakishinikiza kuondoka kwa vikosi vya ulinzi vya Ufaransa nchini humo. **PICHA: DW**

# Matukio ya rushwa yamchefua Papa

**ULAANBAATAR,** Mongolia

KIONGOZI wa Kanisa Katoliki Duniani, Papa Francis, amesifu busara za watu wa Mongolia kwa kudumisha amani na ustahimilivu wa kidini.

Papa Francis aliitahadharisha nchi hiyo juu ya vitendo vya rushwa na uharibifu wa mazingira.

Kiongozi huyo mwenye miaka 86, aliyasema hayo katika ziara yake ya siku tatu nchini Mongolia iliyoanza Ijumaa na alikaribishwa kwa sherehe rasmi iliyokuwa na gwaride la wapanda farasi mbele ya Kasri la serikali.

Akiwa nchini humo alikutana na Rais Ukhnaagiin Khuresukh na kutia saini kitabu cha wageni na kuandika kwamba anatembelea taifa hilo changa lenye historia kongwe la kisasa na lenye utajiri wa tamaduni.

Papa Francis ameitembelea nchi hiyo yenye idadi ndogo zaidi ya waumini wa dhehebu la Kikatoliki duniani ikiwa na wafuasi 1,450.

Awali aliusalimu umati wa watu waliokuwa wamesimama mbele ya sanamu la shaba la Gengis Khan huku vijana wa kikatoliki wakimshangilia.

Safari hiyo pia imewavuta waumini wa Kikatoliki kutoka nchini China ambao walihudhuria pia hafla ya kumkaribisha Papa.

Ziara hiyo ya kidiplomasia ya Papa Francis inalenga kutafuta mshirika asiye na upande wowote, wakati Vatican ikifanya juhudi za kuimarisha uhusiano wake na Mongolia pamoja na mataifa jirani.

Kiongozi huyo alisema, utamaduni wa Washamani na waumini wa Buddha wa kuishi kwa amani na mazingira pamoja na viumbe vilivyomo ndani yake kunaweza kuchangia juhudi za kuinusuru na kuihifadhi sayari ya dunia.



Pamoja na Papa Francis kuipongeza Mongolia, pia alionya dini inaweza kusaidia kujilinda dhidi ya kitisho cha rushwa ambacho ni kikwazo kwa maendeleo ya jamii.

Aliongeza kuwa serikali hazina sababu ya kulihofia kanisa katoliki kwani halina ajenda yoyote ya kisiasa.

Mji wake mkuu wa Ulaanbaatar ni moja kati ya miji yenye kiwango kibaya zaidi cha uchafuzi wa hali ya hewa.

Maofisa wa serikali walikuwa wakituhumiwa kwa vitendo vya rushwa hali iliyosababisha kuzuka kwa maandamano mwaka uliopita.

Sehemu kubwa ya nchi hiyo pia iko hatarini kuwa jangwa kutokana na mabadiliko ya tabianchi, uchimbaji madini na kulisha mifugo mingi kupita kiasi katika baadhi ya maeneo. Ziara ya Papa Francis inadhamiria pia kupeleka ujumbe wa kanisa kwa maeneo ya mbali na yasiyopewa kipaumbele. **DW**

# MASHUJAA FC YATAFUTIA PUMZI LIGI KUU BARA ZIWA TANGANYIKA

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Mashujaa FC kimerejea mazoezini na moja kwa moja kimepelekwa kwenye fukwe za Ziwa Tanganyika, Kigoma kwa ajili ya mazoezi ya kurudisha utimamu wa mwili na pumzi kabla ya kuanza raundi ya tatu ya Ligi Kuu Bara.

**Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mohamed Abdallah 'Bares' (pichani), amesema baada ya mapumziko ni lazima awarejeshee nguvu na pumzi wachezaji wake, hivyo ameanza kwenye fukwe za ziwa hilo hadi pale atakapoona wameiva na baada ya hapo atawahamishia uwanjani.**



"Tuliwapa mapumziko wachezaji wetu, lakini kwa sasa wamerejea na tumeanza kujifua kwenye fukwe za Ziwa Tanganyika hapa, nadhani tuna wiki tatu za mapumziko ya Kalenda ya FIFA, kwa hiyo zinatosha sana kuwafanyisha mazoezi hapa ya utimamu wa mwili, baadaye turudi uwanjani," alisema.

Hata hivyo, Bares amesisitiza kuwa anahitaji mechi angalau tatu za kirafiki na hasa akizilenga timu za nchini Burundi kwa ajili ya kuipa timu yake ushindani.

"Kwangu mimi nahitaji mechi tatu, zinatosha sana, ila nataka zile zenye ushindani na tumeona ndugu zetu wa Burundi timu zao nazo zinajiandaa kwa ajili ya ligi wanaitikia wito wa kutaka kucheza na sisi mechi za kirafiki, kwa hiyo ningependa kucheza na timu za huko, kama itapatikana nafasi ya wao kuja sawa, lakini sisi wenyewe tunaweza kwenda huko kucheza," alisema.

Mpaka sasa Mashujaa iliyopanda daraja na kuanza kucheza Ligi Kuu kwa mara ya kwanza msimu huu, haijapoteza mechi yoyote, ikishinda mchezo wa kwanza mabao 2-0 dhidi ya Kagera Sugar na suluhu dhidi ya Geita Gold FC.

Mashujaa inatarajiwa kucheza dhidi ya Ihefu, Septemba 16, mwaka huu na bado itaendelea kuwa kwenye uwanja wao wa nyumbani, Lake Tanganyika, Kigoma, kwa mechi ya tatu mfululizo.

## UWERFA yazitaka klabu kufuata sheria, kanuni

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

CHAMA cha Mpira wa Miguu Mkoa wa Mjini Magharibi (UWERFA), kimesema kitaendelea kuwa kikali kwa klabu zisizotaka kufuata sheria na kanuni kuelekea msimu huu mpya wa ligi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa chama hicho, Maalim Ahmada, alisema katika kuhakikisha wanasimamia sheria na nidhamu, wameweka mkakati kwa timu zitakazoonekana katika ratiba ya ligi msimu huu ni zile tu zilizokamilisha utaratibu uliowekwa.

Alisema Ligi ya Mkoa wa Mjini Magharibi, ambayo inajumla ya timu 24, imepangwa kuanza kutimua vumbi Septemba 23, mwaka huu, hivyo Septemba 10 ratiba itatolewa kwa klabu zote.

Alisema wiki hii ndio mwisho kwa klabu zote kukamilisha taratibu zilizowekwa ikiwamo kulipa ada ya mashindano, ada ya uwanachama kwa msajili wa vyama vya michezo pamoja na uwanachama wa wilaya zilizotoka klabu husika.




Wanafunzi wa Shule ya Awali na Msingi ya East Africa ya jijini Dodoma wakionesha umahiri wa kucheza mchezo wa karate kwenye mahafali ya shule hiyo mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Shule yaanzisha somo la karate

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KATIKA kuimarisha afya ya akili na mwili kwa wanafunzi Shule ya Awali na Msingi ya East Africa ya jijini Dodoma, imeanzisha somo la mchezo wa karate.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Evarist Runiba, alisema hayo jana wakati akizungumza kwenye mahafali ya kwanza ya darasa la saba ya shule hiyo.

Alisema michezo hiyo ni sehemu ya kuwasaidia kuimarisha afya za wanafunzi wao ili kufanya vizuri katika masomo yao na shughuli mbalimbali za kila siku.

"Shule yetu pamoja na kufundisha masomo mengine, lakini tunafundisha lugha ya kichina na kifaransa, pia tunalo darasa la mchezo wa karate ambalo wanafunzi wote wanapata mafunzo wakiwa hapa shule," alisema.

Alisema katika mchezo huo wa karate wanao walimu waliobobea hali ambayo itasaidia wanafunzi hao kuwa timamu kimwili na kiakili ili kuendelea kufanya vizuri katika masomo yao.

Mgeni rasmi, Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Dodoma, Pilly Mbaga, alisema amefurahishwa na vipaji mbalimbali alivyoviona kwenye shule hiyo.

Alisema ni vema shule zingine ziige mfano huo kwa kutenga muda mzuri wa wanafunzi kucheza na kuimba. Aidha, alisema kuna wanafunzi wenye vipaji mbalimbali kama vilivyoonekana kwenye mahafali hayo na kwamba kama vikiendelezwa, wanaweza kupatikana wasanii wakubwa nchini.

"Mnafanya vizuri sana na mwendelee hivyo hivyo kwenye michezo na burudani kwa sababu hawa wameonyesha vipaji vya aina yake, natoa wito kwa shule zingine kuiga," alisema

Aidha, alisema michezo inawafanya wanafunzi wanakuwa na afya njema hali ambayo pia itachangia kufanya vizuri kwenye masomo na mitihani yao, hivyo walimu wasione kama michezo ni kupoteza muda bila sababu.

"Mbali na masomo ya kawaida wapeni muda wa kucheza kuonyesha vipaji vyao, hawa lazima wapate muda wa kufanya mambo mengine yanayowapa furaha kama michezo," alisema.

## Rugby Wanawake kurindima mwezi ujao

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya Wanawake ya Mchezo wa Rugby, yanatarajiwa kufanyika mwanzoni mwa mwezi ujao au Novemba, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Maendeleo ya Wanawake wa Chama cha Rugby Tanzania, Fatma El Kindly, alisema lengo la mashindano hayo ni kupata timu ya taifa itakayoshiriki michuano ya Afrika hapo mwakani.

"Tutaanza kushiriki mashindano ya kimkoa ambayo tutaanzia Dar es Salaam na kuendelea na mikoa mingine kwa wale watakaofanya vizuri watapata nafasi ya kwenda kushiriki mashindano makubwa," alisema El Kindly.

Alisema kwa upande wa Tanzania walikuwa hawana timu ya taifa, hivyo mwaka huu wamefanikiwa kupata timu nne zenye jumla ya wachezaji 80.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

#### HAALAND MSHAHARA JUU

KLABU ya Manchester City inatarajia kumpa mshambuliaji wa Norway Erling Haaland mshahara mnono wa pauni 600,000 kwa wiki ikiwa ataongeza mkataba wake wa sasa unaomalizika mwaka 2027 wakitaka kumzuia kuhamia Real Madrid au Ligi Kuu Saudia. ***(Daily Star Sunday)***

#### CITY ILIVYOSHINDWA KWA EZE

KATIKA siku ya mwisho ya usajili, Manchester City ilishindwa kutoa dau la pauni milioni 60 kwa ajili ya mshambuliaji wa Crystal Palace, Eberechi Eze, 25, huku 'The Eagles' hao wakitaa pauni milioni 80 kwa ajili ya mchezaji huyo wa England. ***(Sunday Mirror)***

#### POGBA ATAKIWA SAUDIA

KIUNGO wa kati wa Juventus, Paul Pogba, 30, anasakwa na Klabu ya Ligi Kuu Saudia ya Al-Ahli na Al-Ittihad. ***(Gazzetta dello Sport)***

#### RAMOS NAYE ASAKWA

Al-Ittihad pia wamewasilisha pendekezo la kutaka kumsajili, beki wa zamani wa Real Madrid na Paris St-Germain, Sergio Ramos, 37, na wanasubiri jibu kutoka kwa Mhispania huyo ambaye anasakwa na klabu za Uturuki. ***(Fabrizio Romano)***

#### VAN DE BEEK AWANIWA

KLABU ya Galatasaray inaendelea na mazungumzo na Manchester United kuhusu kumsajili kiungo wa Uholanzi, Donny van de Beek, 26, baada ya ofa ya mkopo ya pauni milioni moja kwake kukataliwa katika siku ya mwisho ya uhamisho. ***(Mail on Sunday)***

#### HOJBJERG AANZA KUNYATIWA

GALATASARAY pia wanatarajia kumnunua kiungo wa kati wa Tottenham Hotspur na Denmark, Pierre-Emile Hojbjerg, 28, huku dirisha la uhamisho likiwa bado liko wazi huko Uturuki. ***(Ajansspor, via Sabah)***

#### LLORIS KUSITISHIWA MKATABA

KLABU ya Tottenham Hotspur inaweza kukubali kusitisha mkataba wa golikipa Mfaransa Hugo Lloris, 36, mwaka mmoja kabla ya kumalizika baada ya mchezaji huyo kushindwa kupata timu katika siku ya mwisho ya uhamisho baada ya ofa ya kwenda Newcastle United na Nice kuchelewa kufika mezani. ***(Football Insider)***

#### MASON NA DILI LA LAZIO

RAIS wa Lazio, Claudio Lotito, amesema mshambuliaji wa Manchester United, Mason Greenwood, 21, alitaka kujiunga na klabu hiyo ya Italia, lakini miamba wa Old Trafford hawakukamilisha nyaraka kwa wakati kabla ya Muingereza huyo kujiunga na Getafe kwa mkopo. ***(La Lazio Siamo Noi, via Mail on Sunday)***

#### GRAY AFUATILIWA

MSHAMBULIAJI wa England, Andre Gray, 32, ambaye alizichezea Klabu za Luton Town, Brentford, Burnley na Watford, anafuatiliwa na klabu kadhaa baada ya mchezaji huyo kuondoka Aris Saloniki ya Ugiriki kwa makubaliano. ***(Football Insider)***

#### CARRASCO KWENDA SAUDIA

KIUNGO wa kati wa Atletico Madrid na Ubelgiji, Yannick Carrasco mwenye umri wa miaka 29, atasafiri hadi Saudi Arabia kukamilisha uhamisho wa euro milioni 15 kwenda Al-Shabab. ***(Fabrizio Romano)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# BELLINGHAM APAGAWA KWA SHANGWE KUBWA ZA MADRID

**MADRID,** Hispania

JUDE Bellingham amesema mwitikio wa umati wa mashabiki kwa bao lake la dakika ya 95 katika ushindi wa mabao 2-1 wa Real Madrid dhidi ya Getafe Jumamosi ulikuwa "wakati wa kelele kubwa zaidi kuwahi kuusikia uwanjani."

**Borja Mayoral aliiweka Getafe mbele dakika ya 11 kwenye Uwanja wa Santiago Bernabeu kabla ya Joselu kusawazisha baada ya muda wa mapumziko na Bellingham mwenye umri wa miaka 20, akafunga bao la ushindi dakika za lala salama, bao lake la tano katika mechi nne.**

Matokeo hayo yanamaanisha kuwa Madrid wamechukua pointi nyingi zaidi msimu huu na wanaongoza msimamo wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, wakiwa na pointi 12.

"Ni wakati wa sauti kubwa zaidi ambao nimeusikia kwenye uwanja," alisema Bellingham akiiambia Real Madrid TV. "Siwezi kuamini kuwa mkweli. Wakati umati ulipoimba 'Hey Jude' mwishoni, nilipatwa na butwaa. Nilitaka tu kugeuka na kusimama tuli na kuisikiliza.

> ●●● Ni sauti kubwa zaidi ambazo nimewahi kusikia uwanjani, siwezi kuamini umati...

"Miguu yangu ilikuwa ikitetemeka," alisema Bellingham. "Ninajua kwamba nililetwa kwa nyakati kama hizi. Ni aina ya nyakati ninazojua ninaweza kuifanyia timu hii. Nataka kuendelea kufanya hivyo na kuhakikisha mashabiki wanarudi nyumbani wakiwa na furaha."

Madrid ililipa euro milioni 103 kumnasa kiungo wa kati wa England, Bellingham kutoka Borussia Dortmund msimu huu wa majira ya joto.

Amefunga katika kila mechi kati ya mechi nne za LaLiga hadi sasa: ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Athletic Club, ushindi wa 3-1 dhidi ya Almeria, ushindi wa 1-0 dhidi ya Celta Vigo na sasa kwenye mechi yake ya kwanza ya nyumbani dhidi ya Getafe.

"Yeye ni mtaalamu sana," alisema kocha Carlo Ancelotti alipoulizwa kuhusu kubadilika kwa Bellingham.

"Haiwezi kuwa kwa njia nyingine, weledi katika kikosi hiki uko juu sana. Ana mifano mingi ya kuigwa. Amebadilika vizuri sana."

"Anaweza kufikia mabao 15 bila matatizo yoyote," aliongeza Ancelotti.

"Alifanya hivyo mwaka jana akiwa na Dortmund. Anasimama kwa sababu anasonga vizuri sana bila mpira. Huo ndio ubora wake."

"Ni mchezaji ambaye anajifunza haraka sana," alisema Ancelotti. "Sio lazima kumwambia mambo mara nyingi... Tumemwonesha video za wakati alipocheza huko Dortmund, za vitu tulivyopenda.

"Kilichobadilika ni kwamba anasonga zaidi bila mpira kwenye eneo la wapinzani. Akiwa Dortmund alizoea kucheza katikati ya mstari."

Wapinzani wa Getafe walimsajili Mason Greenwood kwa mkopo kutoka Manchester United siku ya mwisho ya uhamisho.

United ilimwacha fowadi huyo kuondoka kutokana na uchunguzi wa miezi sita kuhusu mwenendo wake, baada ya kushinda kesi ya jinai juu ya madai ya kujaribu kubaka na kushambulia.

SportPesa | LIVE IN PLA

MECHI KALI
CAMBRIDGE UTD
VERSUS
READING
1 | 2.32
X | 3.29
2 | 2.89

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# KANE KWENDA BAYERN MUNICH KUTAISAIDIA ENGLAND - SOUTHGATE



**LONDON,** England

GARETH Southgate anaamini kuwa England inaweza kufaidika kutokana na uhamisho wa Harry Kane kwenda Ujerumani - haswa ikiwa nahodha wake huyo atajinyakulia taji la kwanza katika maisha yake ya soka akiwa Bayern Munich.

Kane mwenye umri wa miaka 30, aliondoka katika klabu yake ya utotoni, Tottenham Hotspur na kwenda kule kwenye dimba la Allianz Arena kwa mkataba ambao uligharimu pauni milioni 100.

Alikuwa akihusishwa na kuondoka Spurs kwa misimu michache iliyopita, sasa mustakabali wa Kane na Southgate anafurahi kumuona akikipiga akiwa Bayern.

“Kwa hakika nafikiri kwa mtazamo wangu ni vema hatima yake iwe imetulia sasa kwa miaka michache ijayo,” alisema kocha huyo wa England.

“Nadhani uwezekano huo unaweza kuwa usumbufu kwa wachezaji. Lakini ni vizuri kwake kwamba lazima aende kucheza katika klabu mpya. Amekuwa kwenye klabu moja kwa muda mrefu.

“Kuwa na mabadiliko inamaanisha lazima ufurahie wachezaji wenzake wapya, wafanyakazi wapya, mashabiki wapya na pia kuna uzoefu wa maisha na kuzoea nchi mpya. Nadhani kuna mazuri mengi huko.”



## Ronaldo afikisha mabao 85

**RIYADH,** Saudi Arabia

CRISTIANO Ronaldo alisherehekea kufikisha mabao 850 katika maisha yake ya soka wakati akiisaidia Al Nassr kushinda 5-1 dhidi ya Al Hazem kwenye Ligi ya Saudi Arabia, Jumamosi.

Ronaldo alifunga bao lake la sita katika michezo yake mitatu na kutoa pasi mbili za mabao wakati Al Nassr wakiandikisha ushindi wa tatu mfululizo kwenye ligi hiyo, huku Sadio Mane pia akifunga bao.

“Uchezaji mwingine mzuri wa timu! Tunaendelea kuboresha. Twende Al Nassr FC ... mabao 850 ya kazi na bado tunayahesabu!” Alianadika Ronaldo mwenye umri wa miaka 38 katika mtandao wake wa kijamii wa Instagram.

Ronaldo sasa amefunga mabao 26 katika michezo yake 30 ya kwanza kwenye mashindano yote akiwa na Al Nassr, ikiwa ni moja tu pungufu ya idadi aliyofunga katika mechi sawa na l mwanzoni mwa maisha y ya soka kule Real Madrid

Mpinzani wake wa m mrefu, Lionel Messi kwa ana mabao 818 katika r sha yake ya soka.

Baada ya Al Nassr poteza mechi zao mbil kwanza za ligi msimu l washindi wa pili wa ms uliopita, ambao wamefu mabao 14 katika mich yao mitatu iliyopita, wamepitwa pointi nne vinara Al Hilal.

CHEZA USHINDE KASINO

# PIALALI, MAIGWISA WACHEZEA KICHAPO NAMIBIA WBO AFRIKA

**Na Saada Akida**

MABONDIA wawili wa Ngumi za Kulipwa Tanzania, Idd Pialali na Joseph Maigwisa, wameshindwa kutamba katika mapambano ya kuwania mikanda ya ubingwa wa WBO Afrika baada ya kupoteza kwa vichapo vya pointi na TKO nchini Namibia.

Pialali alikuwa akiwania mkanda ubingwa wa WBO Afrika katika uzani wa Super Walter, ambapo alipoteza pambano hilo la raundi 12 kwa pointi dhidi ya Charles Shinima wa Namibia.

**Wakati Joseph Maigwisa akipoteza kwa TKO raundi tano ya pambano la kuwania mkanda wa WBO Afrika katika uzani wa Super Middle dhidi ya Paulinus Ndjolonimu wa nchini humo.**

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha wa Pialali, Edward Lyakwipa, alisema Maigwisa amepoteza pambano kwa TKO ambapo mwamuzi aliona bondia kupokea ngumi kali licha ya kuwa tayari kengele ya mapumziko imelia kitu ambacho kiliwashangaza.

Alisema kwa Pialali, alianguka katika raundi ya kwanza kabla ya kukaa sawa na kuendelea na pambano hilo ambalo lilikuwa gumu kwa upande wake hali iliyosababisha kocha wake kumpongeza kutokana kuonesha ukomavu mkubwa wa kuweza kumaliza pambano kutokana na mpinzani aliyekutana naye.

"Tulifanya maandalizi mazuri, lakini mabondia wetu hawakuweza kufanya vizuri kwa wote wawili kupoteza, wapinzani walikuwa vizuri na kuwazidi mbinu na kushindwa kureje nyumbani na mkanda wowote," alisema kocha huyo.

Aliongeza kuwa wamerejea nyumbani kujipanga na mapambano mengine yaliyopo mbele yao kuhakikisha wanafanya vizuri kwa kuwa tayari wameona makosa yao.

## Mama Aziz Ki amwanika

INATOKA UKURASA 24

Akieleza maisha ya kijana wake, alisema hakumaliza shule kwa sababu ya mpira wa miguu ambao alianza kucheza akiwa na miaka saba tu, huku mara kwa mara akiwa anatoroka au kutega shule.

"Naweza kusema alizaliwa ili acheze mpira, alianza kupenda soka ana miaka mitano tu, baba yake alikuwa anampenda mchezaji mmoja raia wa Morocco anaitwa Aziz Bouderbala na ndilo alilopewa yeye, alikuwa akiamka asubuhi kabla ya kunywa chai anakwenda kucheza uwanjani, baadaye ndiyo anakwenda shule, watu wakaanza kutambua kipaji chake na ilikuwa ni kipindi ambacho anasoma, ila nikaja kugundua kuwa kuna wakati anakwenda shule, lakini wakati mwingine anatega, anatoroka kwenda kucheza mpira," alisema.

Alisema mwaka wa pili akiwa shule ya sekondari alikataa kuendelea na masomo kwani soka lilikuwa kwenye damu.

"Mwaka wa pili akiwa sekondari akaniambia kuwa hataki shule, anataka kuendelea kucheza soka, nikamwambia hivyo vitu vyote vinatakiwa kwenda sambamba, utasaini vipi mikataba wakati huna elimu?

Kwa sababu alisimamia msimamo wake, nikamuacha afanye anavyotaka kwa sababu aliniambia ana maono makubwa kuhusu soka, alipofikisha miaka 17 alikwenda Hispania na Ufaransa kwa ajili ya kucheza soka na kurejea baadaye kwenye kikosi cha Asec Mimosas," alisema.



Luis Miquissone

## Mastaa Simba waionya

INATOKA UKURASA 24

Mkapa).

Alisema wanawakaribisha Al Ahly na kuwataka kukumbuka kilichowapata mara ya mwisho wakicheza nao, kitajirudia kwa mara ya pili kwa kuendeleza walipoishia.

"Waje, tunawakaribisha kwa Lupaso, wanapokuja wakumbuke kilichowatokea mara ya mwisho, kwa sababu kila anayekuja nyumbani hawezi kuondoka hivi hivi, maandalizi yanaendelea vizuri.

"Tumejiandaa vizuri, malengo ya timu msimu huu ni kuona tunafanya vizuri kila michuano iliyopo mbele yetu, kutwaa mataji ya ligi ya ndani, kuvuka hatua ya robo fainali na kucheza nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, lakini pia kufanya vizuri Afrika Football League kwa kuanza kumpiga Al Ahly hapa nyumbani," alisema Tshabalala.

Simba wanaendelea na mazoezi ya kujiandaa na mchezo wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Power Dynamos ya Zambia, utakaochezwa Septemba 16, mwaka huu nchini humo kabla kurudiana jijini Dar es Salaam Septemba 29, mwaka huu.


SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" – NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" – NI TIMU KUTOKA SARE
"2" – NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 04/09/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 2753 | Guangzhou Evergrande vs Anhui Litian | 3.31 | 3.26 | 2.04 |
| 16:00 | 3557 | Raufoss IL 2 vs Molde FK 2 | 6.40 | 5.40 | 1.28 |
| 16:00 | 4746 | Charlton U23 vs Birmingham U21 | 1.79 | 4.27 | 3.25 |
| 16:00 | 5480 | Kelantan United FC vs Kuching FA | 2.44 | 3.22 | 2.57 |
| 16:00 | 5638 | Millwall U23 vs Crewe U23 | 1.27 | 5.69 | 7.31 |
| 17:00 | 1383 | FK Tyumen vs Arsenal Tula | 2.14 | 3.14 | 3.09 |
| 17:00 | 1691 | CA Belgrano vs CD Godoy Cruz | 1.35 | 4.20 | 7.40 |
| 17:00 | 3687 | FC Struga Trim Lum vs FK Tikves Kavadarci | 1.63 | 3.67 | 4.68 |
| 17:00 | 4593 | Arsenal FC Reserve vs CA River Plate (Arg) | 3.87 | 3.16 | 1.90 |
| 17:30 | 2253 | NK Dubrava vs NK Dugopolje | 2.10 | 3.18 | 3.13 |
| 18:00 | 2716 | San Lorenzo de Almagro W vs Estudiantes de La Plata | 1.39 | 4.30 | 6.75 |
| 18:00 | 5478 | Follo vs Tromso IL 2 | 1.14 | 7.00 | 10.00 |
| 18:30 | 1206 | Botosani vs Hermanstadt | 3.03 | 2.98 | 2.36 |
| 19:00 | 1879 | Djurgaardens IF W vs Kristianstads W | 4.28 | 4.08 | 1.61 |
| 19:00 | 3020 | JK Tammeka Tartu II vs Nomme JK Kalju | 2.22 | 3.60 | 2.55 |
| 19:00 | 3564 | Bnei Yehuda vs SC Kfar Qasem | 2.38 | 3.17 | 2.91 |
| 19:00 | 4370 | Vindbjart vs Odds BK 2 | 1.87 | 3.90 | 3.05 |
| 19:00 | 5497 | Sectzya Nes Ziona vs El Fahem | 2.49 | 3.00 | 2.90 |
| 19:15 | 5980 | Kotwica Kolobrzeg vs Radunia Stezyca | 1.95 | 3.26 | 3.57 |
| 19:30 | 4049 | Rodina Moscow vs Torpedo Moscow | 2.11 | 3.12 | 3.17 |
| 20:00 | 1269 | Sandefjord Fotball 2 vs Eik-Tonsberg | 5.20 | 5.00 | 1.38 |
| 20:00 | 2237 | Oppsal IF vs Skeid Fotball 2 | 2.09 | 3.89 | 2.67 |
| 20:00 | 2305 | Start 2 vs Mandalskameratene | 3.32 | 3.98 | 1.79 |
| 20:00 | 2685 | Naestved BK vs HB Koge | 1.77 | 3.53 | 3.84 |
| 20:00 | 3592 | Aaskollen vs Fredrikstad FK 2 | 2.57 | 3.84 | 2.17 |
| 20:00 | 3636 | Skjetten vs Stabaek Fotball 2 | 2.25 | 3.59 | 2.58 |
| 20:00 | 4650 | FC Trollhattan vs Ljungskille | 1.37 | 4.64 | 6.05 |
| 20:00 | 5297 | FC Ashdod vs Beitar Jerusalem | 2.68 | 3.24 | 2.34 |
| 20:00 | 5398 | FK Zeleznicar Pancevo vs Cukaricki St | 4.24 | 3.48 | 1.70 |
| 20:00 | 5853 | Halsen IF vs Mjondalen 2 | 1.97 | 4.00 | 2.83 |
| 20:00 | 5927 | Frigg vs Lillestrom SK 2 | 1.15 | 7.25 | 9.87 |
| 20:30 | 1281 | Grindavik W vs Vikingur Reykjavik W | 6.50 | 5.28 | 1.32 |
| 21:00 | 2635 | Zrinjski Mostar vs Siroki Brijeg | 1.42 | 4.19 | 6.34 |
| 21:00 | 3520 | HFX Wanderers FC vs York United FC | 2.00 | 3.35 | 3.30 |
| 21:00 | 5911 | Ham-Kam 2 vs Brumunddal | 1.73 | 4.00 | 3.40 |
| 21:15 | 3379 | Rosario Central W vs Club El Porvenir | 1.19 | 5.48 | 13.20 |
| 21:30 | 1264 | Deportivo Espanol vs Berazategui | 2.13 | 3.00 | 3.36 |
| 21:30 | 5876 | Sepsi Osk vs UTA Arad | 1.69 | 3.59 | 4.52 |
| 21:45 | 1066 | Vicenza vs Albinoleffe | 1.59 | 3.81 | 5.64 |
| 21:45 | 1545 | Fiorenzuola vs Renate | 2.53 | 3.13 | 2.82 |
| 21:45 | 1685 | Alessandria vs Novara | 3.92 | 3.35 | 1.94 |
| 21:45 | 2157 | Pro Vercelli vs AC Lumezzane | 2.06 | 3.24 | 3.61 |
| 21:45 | 2513 | Mantova vs Padova | 2.59 | 3.15 | 2.73 |
| 21:45 | 3152 | US Pergolettese vs AC Pro Sesto | 2.24 | 3.08 | 3.35 |
| 21:45 | 3344 | Triestina vs Trento Calcio 1921 | 2.04 | 3.08 | 3.92 |
| 21:45 | 5730 | Chelmsford vs Hemel Hempstead | 1.64 | 3.67 | 4.59 |
| 22:00 | 2586 | Cambridge Utd vs Reading | 2.32 | 3.29 | 2.89 |
| 22:00 | 5788 | FC Martigues vs Red Star | 2.90 | 3.16 | 2.36 |
| 22:15 | 3948 | Afturelding Mosfellsbaer W vs Fram | 1.55 | 4.20 | 4.30 |
| 23:15 | 3492 | Cesar Vallejo vs Atletico Grau | 1.91 | 3.34 | 3.49 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatatu Septemba 4, 2023

Nipashe





Ronaldo afikisha mabao 850 UKURASA 22


# Mastaa Simba waionya Al Ahly AFL

●●● Ni baada ya droo, Miquissone, Tshabalala wakumbusha ya Ligi Mabingwa kwa...

**Na Saada Akida**

BAADA ya Simba kumjua mpinzani wake kwenye michuano ya itakayoshirikisha ya klabu nane bora zaidi Afrika, African Football League (AFL), mastaa wa Wekundu wa Msimbazi hao, wametoa tahadhari kwa Al Ahly na kudai kilichowakuta Februari 23, 2021, kitawarudia tena katika mchezo wa ufunguzi Oktoba 20, mwaka huu.

**Katika droo ya michuano hiyo iliyochezwa jijini Cairo Misri, Jumamosi iliyopita, TP Mazembe ya DR Congo yenyewe itavaana na Esperance ya Tunisia na mshindi wa mechi hiyo atacheza nusu fainali dhidi ya mshindi kati ya Enyimba na Wydad Casablanca ya Morocco.**

Mchezo wa Simba dhidi ya Al Ahly, ndio utakaokuwa wa ufunguzi ukipigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam Oktoba 20, mwaka huu na kurudiana nchini Misri siku nne baadaye na mshindi wa jumla atakutana na mshindi kati ya Petro de Luanda ya Angola dhidi ya Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini.

Klabu ya Simba inakuwa timu pekee kutoka Ukanda wa Afrika Mashariki itakayoshiriki michuano hiyo inayoanza kwa mara ya kwanza msimu huu.

Simba ambayo imekuwa na rekodi nzuri ikicheza michuano ya kimataifa ngazi ya klabu nyumbani katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Februari 23, 2021, kwenye mechi ya hatua ya makundi ikiwa Kundi A pamoja na Al Ahly, ilibuka na ushindi wa bao 1-0 uwanjani hapo dhidi ya Wamisri hao kabla ya kwenda ugenini na wenyeji kupata ushindi kama huo.

Ushindi huo unawafanya wachezaji kuamini inawezekana tena kama watajipanga vema kuelekea michuano hiyo inayoelezwa kuwa na utajiri mkubwa zaidi kwa ngazi ya klabu Afrika.

Katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Mkapa dhidi ya Al Ahly, bao hilo pekee lilifungwa na Luis Miquissone, ambaye baada ya msimu huo kumalizika alisajiliwa na wababe hao wa Misri kabla ya msimu huu kurejea tena Simba.

Akizungumzia mchezo huo, Miquissone alisema itakuwa mechi nzuri kwa sababu anaifahamu timu hiyo na anaimani utakuwa mchezo wa ushindani mkubwa kwa kuwa wamejipanga kufanya vizuri.

"Nakutana na timu ambayo nimetoka kuitumikia, nawafahamu utakuwa mchezo mzuri, tumejiandaa vizuri kwa michezo yote ikiwamo dhidi ya Al Ahly timu yangu ya zamani.

"Mashabiki watarajie kuona mchezo mzuri kwa sababu timu yetu iko vizuri na malengo yaliyopo ni kufanya vizuri kila mechi, ikiwamo michuano hiyo AFL," alisema nyota huyo.

Naye nahodha msaidizi wa Simba, Mohammed Hussein 'Tshabalala', alisema wapinzani wao wanatambua kilichowatokea mara ya mwisho kwenye uwanja huo wa 'Lupaso' (Benjamin


INAENDELEA UKURASA 23




Aziz Ki

## Mama wa Aziz Ki amwanika Yanga SC

**Na Adam Fungamwango**

MAMA mzazi wa kiungo mshambuliaji wa Yanga, Stephane Aziz Ki, Ki Sanata, amefichua kuwa mwanawe huyo huduma yake ilihitajika na Simba msimu uliopita, lakini alikataa kutokana na aina ya uchezaji wa timu hiyo kuwa hauendani naye.

Akihojiwa na chaneli ya klabu hiyo, Bi. Ki Sanata, alisema Aziz Ki aliiona Simba ikicheza katika mechi ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, Februari na Machi 2022, alipokuwa akiitumikia Asec Mimosas na kucheza mechi mbili za nyumbani na ugenini dhidi ya Wekundu wa Msimbazi hao.

Pia mama huyo aliweka hadharani kuwa mchezaji huyo alihitajika na timu mbili za Tanzania, moja ya Misri na nyingine Morocco, lakini mwisho wa siku akaamua kwenda kuichezea Yanga.

"Alipokuwa Asec Mimosas, klabu nne zilikuwa zinamtaka, Misri, Morocco na klabu mbili za Tanzania, aliwahi kucheza dhidi ya Simba hapa, lakini hakupenda aina yao ya uchezaji na akaanza kuangalia aina ya uchezaji wa Yanga akaipenda, akaona aina yao inaendana na uchezaji wake," alisema Bi. Ki Sanata.

Maelezo haya yanamaliza uvumi, tetesi au malumbano kama Simba ilikuwa inamtaka mchezaji huyo au la.

Wakati akisajiliwa na Yanga, ilidaiwa kuwa Simba ilikuwa ya kwanza kumtaka, na hata baada ya kusajiliwa, baadhi ya viongozi wa timu hiyo walikataa katakata kuwa hawajawahi kutuma ofa au kumtaka mchezaji huyo.

Mama Aziz Ki alisema kijana wake hakufuata pesa Tanzania kwani alikuwa na ofa nyingine kubwa, lakini kwa sababu ameshacheza klabu mbalimbali ndani na nje ya bara la Afrika alichofuata ni kucheza kwa uhuru na amani kwani kuna matatizo mengi katika baadhi ya nchi ikiwamo upendeleo na ubaguzi.

"Mtoto aliniambia anataka kwenda kucheza akiwa huru na amani, kuna nchi zingine zina ubaguzi," alisema.


INAENDELEA UKURASA 23



GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042



9 770856 541002 >